# JARIDA LA WAKILI MKUU

ISSN 2686 | Toleo la Kumi na Tano | Agosti - Novemba, 2025



## DKT. ALLY POSSI
### WAKILI MKUU WA SERIKALI

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

**Salmin Hezron Kigondo**
Mtaalam

## Wajumbe

**Saddy Rashid Sevingi**
Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usuluhishi

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Huduma za Maktaba

**CPA(T) Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# TAHARIRI

## Prisca Jackson Ulomi

Mhariri Mkuu



Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhila aliyetuwezesha kufika siku hii ya leo tukiwa wazima wa afya. Naomba kutumia fursa hii kuendelea kuwashukuru wasomaji wetu na wadau kwa kuendelea kutuunga mkono kwa namna moja au nyingine kuendelea kuzalisha jarida bora na lenye mvuto linalotolewa ili kuendelea kuhabarisha umma kuhusu namna Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) inavyotekeleza majukumu yake.

Toleo la 15 la Jarida la Wakili Mkuu limeendelea kuwa daraja muhimu la kuakisi dhamira ya dhati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uwazi na ufanisi mkubwa, sambamba na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu kazi na mchango wa Ofisi hii muhimu katika kulinda maslahi mapana ya Serikali na taifa kwa ujumla.

Katika kipindi hiki, OWMS imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Ushirikiwa Ofisi katika maonesho ya Sabasaba na Nanenane umeendelea kuwa chachu ya kuitangaza Ofisi kwa wadau wake wa ndani na nje ya nchi. Kupitia maonesho haya wananchi na wadau mbalimbali wamepata fursa ya kuelewa kwa undani zaidi utekelezaji wa majukumu ya OWMS, mafanikio yake na mchango wake katika kuhakikisha Serikali inaendelea kushinda mashauri katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kulinda mali na rasilimali za Taifa kwa ujumla.

Aidha, ziara ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa mbalimbali nchini imeendelea kuleta matokeo chanya katika kuboresha utendaji kazi wa Ofisi. Ziara hiyo imekuwa fursa ya kufuatilia na kukagua utendaji kazi katika Ofisi za mikoani, kujenga uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa majukumu ya kisheria na kuongeza ari ya watumishi katika kuhakikisha mashauri yote yanayoihusu Serikali yanaendeshwa kwa ufanisi, weledi na kwa wakati. Hatua hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kiwango cha ushindi wa Serikali katika mashauri mbalimbali, jambo linalochochea utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kasi na ufanisi zaidi kwa manufaa ya umma.

Vilevile, Toleo hili limebeba kwa kina taarifa kuhusu mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na OWMS kwa Mawakili wa Serikali. Mafunzo haya yamelenga kuwajengea uwezo na uelewa mpana katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi ili kuhakikisha mashauri yote yatakayofunguliwa baada ya uchaguzi mkuu yanaendeswa kwa ufanisi, weledi na uadilifu wa hali ya juu ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati. Jarida la Wakili Mkuu ni kielelezo cha mwendelezo wa jitihada za OWMS katika kuimarisha utendaji, kuongeza uwazi na kuboresha mawasiliano kati ya Ofisi na wadau wake. Hivyo, ni matumaini yetu kuwa kupitia taarifa zilizomo kwenye jarida hili, wasomaji wataendelea kupata uelewa mpana wa kazi na mchango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kujenga Taifa lenye misingi imara ya utawala wa sheria kwa maendeleo endelevu.

Nikutakie usomaji mwema wa Jarida hili!

# Dawati la Mwenyekiti

## Alice Edward Mtulo

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali



Niwakaribishe wasomaji wetu katika Toleo la 15 la Jarida la Wakili Mkuu. Toleo linaendelea kuonesha dhamira thabiti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uwazi na ufanisi mkubwa hususan katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

OWMS itaendelea kusimamia mashauri hayo kwa weledi na ufanisi zaidi ikiwa ni sehemu ya mchango wake muhimu katika kuhakikisha Serikali inaendelea kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika kuimarisha utawala wa sheria nchini. Kuimarika kwa ufanisi katika uendeshaji wa mashauri kumeendelea kuwa nguzo muhimu katika kusaidia Serikali chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuendeleza na kuimarisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo yenye lengo la kuwaletea wananchi maendeleo endelevu.

Kupitia usimamizi bora wa mashauri, Serikali imeendelea kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika kulipa wadai iwapo ingeshindwa mahakamani, fedha ambazo sasa zinaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo.

Hatua itakayoendelea kuimarisha mahusiano ya nchi kimataifa na kuchechemua uchumi wa nchi mara baada ya kukamilika kwa miradi hiyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2050, inayolenga kujenga uchumi imara na ustawi wa wananchi wake.

Aidha, kama tunavyofahamu kuwa Oktoba 29, 2025 nchi yetu imefanya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, hivyo nawasihi wadau wote wa Serikali kwa ujumla kuendelea kujijengea uelewa na umahiri katika sheria na kanuni za usimamizi wa mashauri ya uchaguzi kwa kuwa ni muhimu mashauri haya yakaendeshwa kwa weledi, haki na kwa wakati ili kuhakikisha viongozi waliochaguliwa wanatekeleza majukumu yao mapema kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo bila ucheleweshaji. Vilevile, napenda kutumia jukwaa hili muhimu kuwasihi watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla, kutumia haki yao ya msingi ya kikatiba kwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ili kuchagua viongozi makini, waadilifu na wazalendo watakaoendelea kulitumikia Taifa letu kwa bidii na kuhakikisha tunasonga mbele katika safari ya maendeleo endelevu ili kwa pamoja tuendelee kuijenga Tanzania yenye misingi imara ya utawala wa sheria, uwajibikaji na maendeleo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mungu ibariki Afrika,
Mungu ibariki Tanzania,
Mungu ibariki Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali!

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. **06** | Mawakili wa Serikali Watakiwa Kufanya Utafiti Kabla ya Kuendesha Mashauri |
| UK. **10** | Katibu Mkuu Maswi Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kusimamia Mashauri kwa Weledi |
| UK. **12** | Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Alipongeza Jeshi la Magereza |
| UK. **14** | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapokea Kompyuta Mpakato 30 |
| UK. **16** | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawafikia Wananchi 826 Maonesho ya Nanenane |
| UK. **18** | Watumishi wa Serikali Wahimizwa Kupima Afya Zao |
| UK. **21** | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Manyara Yakabidhiwa Gari |
| UK. **24** | Zingatieni Sheria, Taratibu na Kanuni za Manunuzi |
| UK. **26** | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yasogeza Huduma Karibu na Wananchi |
| UK. **28** | OWMS Yapunguza Gharama Kwa Wadau ya Kupata Ushauri wa Kisheria |
| UK. **30** | Serikali Yaahidi Sheria Rafiki kwa Wawekezaji Kufanikisha Dira 2050 |
| UK. **34** | Wakili Mkuu Sports Club Yaibagaza Osha Sports Club |
| UK. **36** | Timu ya Kamba ya Wanawake ya OWMS Yaibuka Kidedea |
| UK. **38** | Wakili Mkuu wa Serikali Ampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| UK. **40** | Hotuba ya Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan Baada ya Kuapishwa 2025 |
| UK. **45** | Hotuba ya Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan Wakati wa Kufungua Bunge la 13 |
| UK. **72** | Wajibu wa Mawakili wa Serikali Katika Kuiwakilisha Serikali Katika Mashauri |

# Mawakili wa Serikali Watakiwa Kufanya Utafiti Kabla ya Kuendesha Mashauri




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao kwa lengo la kuwajengea uwezo yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wametakiwa kufanya utafiti kabla ya kuendesha mashauri ya Serikali ili waweze kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri hayo kwa ufanisi hatua itakayosaidia kuiletea nchi yetu maendeleo.

Wito huo umetolewa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu namna ya kuendesha mashauri ya uchaguzi yaliyofanyika Jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo hayo, Dkt. Possi amesema kuwa kufanya utafiti wa kina utawasaidia Mawakili hao kufahamu sheria, kanuni, maamuzi ya

*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



Mahakama yaliyopita na maandiko ya kisheria kuhusu mashauri mbalimbali wanayotarajia kuendesha na yanayoendelea katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aliongeza kuwa kufanya utafiti wa kutosha kabla na wakati wa kuendesha mashauri kunampa wakili wa Serikali ujasiri na uhakika wa kushinda shauri husika mahakamani. Hivyo, kuisaidia Serikali kuokoa fedha ambazo zingelipwa iwapo Serikali ingeshindwa. Aidha, fedha hizo zitatumika kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo anga, reli, miundominu ya barabara, afya, kilimo na elimu nchi nzima.

Alifafanua kuwa utafiti mzuri utawawezesha Mawakili wa Serikali kubashiri hoja zinazoweza kuibuliwa na Mawakili wa upande wa pili, hatua itakayowaweka kwenye nafasi nzuri ya kujibu hoja hizo kwa ufasaha na kushinda mashauri Mahakamani.

Kuhusu masuala ya kuzingatia kabla ya kuingia Mahakamani, Dkt. Possi alieleza kuwa, ni muhimu kufanya maandalizi ya kina ikiwa ni pamoja na kuandaa mashahidi wake vizuri, kukamilisha vielelezo vyote vinavyohitajika kwa wakati, kuandaa na kupangilia hoja za kisheria na kuwa na mkakati madhubuti katika kuuliza maswali yatakayoleta matokeo chanya kwa wakati.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili hao yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Kigoma kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu George Kalenda akichangia mada wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Robert Makaramba akitoa mada kwa Mawakili wa Serikali wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

Alieleza kuwa ni muhimu kuandaa nyaraka zote za kisheria kwa usahihi, kwa kuzingatia matumizi rasmi ya lugha na viwango vya kitaalamu ili kuepusha mapungufu ya kisheria na kiufundi, ikiwa ni pamoja na kuhakiki nyaraka za shauri husika kabla ya kuziwasilisha Mahakamani.

Kiongozi huyo amewataka Mawakili wa Serikali kuzingatia mabadiliko ya sheria mara kwa mara ili kwenda na wakati kwa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu sheria na kanuni mpya zilizopo ili kuepuka kutumia kanuni na sheria zilizopitwa na wakati ambazo zinaweza kuathiri uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi au mashauri mengine ya umma na hivyo kuinyima Serikali kupata haki mahakamani.

Aidha, amewasihi Mawakili wa Serikali kuendesha mashauri hayo kwa kufuata maadili ya uwakili na kuwa waadilifu wakati wote wanapokuwa Mahakamani na kuendesha mashauri kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa ili kuepuka mgongano wa maslahi unaoweza kujitokeza katika kuhakikisha wanalinda maslahi mapana ya Serikali.

Kiongozi huyo amewaasa Mawakili hao kuhakikisha wanashirikiana wakati wote ndani na nje ya Mahakama pamoja na maafisa wa Serikali, na mashahidi ili kuhakikisha shauri linaendeshwa kwa uratibu na mshikamano hatimaye Serikali iweze kupata haki yake kwa wakati.

Katika hatua nyingine, Dkt. Possi amewataka Mawakili wa Serikali kote nchini kushiriki zoezi la kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2025 ili waweze kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka kuanzia Rais, Wabunge na Madiwani ili kulileta taifa letu maendeleo.

Kwa upande wake Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo amesema kuwa uwepo wa mafunzo haya kutawawezesha Mawakili wa

*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



Serikali kupata uelewa mpana wa sheria za uchaguzi na mabadiliko yake pamoja na kujifunza mbinu mbalimbali za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi nchini.

Ameeleza kuwa mafunzo haya ni mwendelezo wa mafunzo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Akizungumzia faida zilizopatikana kutokana na uwepo wa mafunzo haya, Bi. Mtulo ameeleza kuwa mwaka 2024 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mafunzo kama hayo ambayo yaliwajumuisha Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo yalisaidia kuleta matokeo chanya katika uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wa Serikali za mitaa yaliyofunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini.

Alifafanua kuwa baada ya uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2024, Mashauri ya uchaguzi 65 yalifunguliwa kupinga uendeshaji na matokeo ya chaguzi hizo kupitia mafunzo madhubuti waliyopata Mawakili wa Serikali waliweza kusimama imara katika kuendesha mashauri hayo hatua iliyopelekea Serikali kushinda mashauri yote 65 ambayo yaliendeshwa mahakamani.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyeketi katikati) akiwa na Mawakili wa Serikali baada ya kufungua Mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Ndugu Selemani Mtibora akitoa mada kuhusu kanuni za uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akimsikiliza Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Ndugu Selemani Mtibora (hayuko pichani) akitoa mada kwa Mawakili wa Serikali kwenye mafunzo ya Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# Katibu Mkuu Maswi Aipongeza OWMS Kwa Kusimamia Mashauri Kwa Weledi




*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu Eliakimu Maswi akipitia Jarida la Wakili Mkuu alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho hayo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepongezwa kwa kuendelea kusimamia kwa weledi mashauri ya madai na usuluhishi hatua ambayo imesaidia Serikali kuongeza kasi katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Pongezi hizo zimetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu Eliakim Maswi alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya 49 ya Biashara (Sabasaba) yaliyofanyika Julai, 2025 katika viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.

Ndugu Maswi alisema kuwa uwepo wa weledi na ufanisi katika uendeshaji wa mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi umeongeza kasi katika kupunguza na kutatua migogoro ya kisheria kwa njia ya majadiliano badala ya kutumia muda mrefu kusikiliza mashauri mahakamani.

Ameongeza kuwa fedha zinazookolewa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zime-

kuwa zikitumika kujenga miradi mikubwa ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia wananchi kote nchini katika kufanya shughuli zao za kujiletea maendeleo kwa urahisi.

Akiitaja miradi mikubwa inayotekelezwa nchini, ndugu Maswi amesema kuwa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115 linalojengwa mto Rufiji, reli ya kisasa ya SGR, bwawa la kidunda, vituo vya afya, miradi ya barabara, elimu, ujenzi wa meli Ziwa Victoria pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa unaojengwa Msalato Jijini Dodoma.

Ameongeza kuwa kukamilika kwa miradi hii kutachochea kasi ya wananchi katika kujiletea maendeleo kwenye nyanja ya uchumi na kijamii kwa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Aidha, Maswi ameipongeza Ofisi hiyo kwa kuendelea kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wanaotembelea banda la Ofisi hiyo katika Maonesho ya Sabasaba kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuelewa haki zao na namna ya kuzitekeleza kupitia mfumo wa kisheria ikiwemo mashauri ya madai, usuluhishi, mashauri ya katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora wa Ofisi hiyo, Bi. Mercy Kyamba amesema kuwa ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho hayo ya Sabasaba ni mwendelezo wa Ofisi hii kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuendelea kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi wanaotembelea banda la Ofisi hiyo.

Bi. Kyamba ameongeza kuwa Maonesho ya Sabasaba yatasaidia kujenga na kuongeza mahusiano na wadau hatua itakayosaidia kutangaza majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa taasisi za Serikali ambazo ndio wadau muhimu katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi.

Maonesho ya 49 ya kimataifa ya Kibiashara yalianza tarehe 28 Juni 2025 na kufunguliwa tarehe 7 Julai, 2025 na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.




*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu Eliakimu Maswi akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




*Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba akitoa maelezo kuhusu tofauti ya utekelezaji wa majukumu kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwananchi aliyetembelea banda la Ofisi hiyo wakati wa Maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipatiwa maelezo kuhusu kazi za mikono zinazopatikana ndani ya Banda la Magereza alipotembelea banda hilo wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Alipongeza Jeshi la Magereza

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo amelipongeza Jeshi la Mageraza nchini kwa kazi kubwa wanayofanya katika kukuza na kuendeleza shughuli za ujasiriamali hatua ambayo inasaidia kuinua uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Bi. Mtulo alitoa pongezi hizo tarehe 07 Agosti, 2025 alipotembelea banda la Maonesho la Jeshi la Magereza katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Nanenane vilivyopo Nzuguni Jijini Dodoma.

Kupitia ziara hiyo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alipata fursa ya kujionea bidhaa mbalimbali zinazotolewa na taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na mazao mbalimbali kama mbogamboga, nafaka, viatu



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipatiwa maelezo kuhusu bidhaa na huduma mbalimbali zinazopatikana ndani ya Banda la Magereza alipotembelea banda hilo wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



na mikanda, kazi za mikono na ufugaji ambazo zote zimetengenezwa na wafungwa waliopo kwenye Magereza mbalimbali nchini.

Bidhaa nyingine zinazotengenezwa na wafungwa hao ni samani mbalimbali za majumbani na maofisini kama vile vitanda, makochi, meza, viti, mikoba, vikapu,viatu pamoja na shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama, sungura, mbuzi, kuku na bata mzinga.

Ameongeza kuwa uwepo wa shughuli hizo katika Magereza mbalimbali nchini kunasaidia kujenga taifa lenye wataalam na ujuzi kwa vijana na wananchi wa rika zote hasa kwa wafungwa wanapotoka gerezani baada ya kumaliza kutumikia vifungo vyao walivyohukumiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Katika hatua nyingine kiongozi kuyo amesema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kushiriki maonesho ya Wakulima, Wafugaji na Uvuvi kwa lengo la kuendelea kujenga na kuimarisha mahusiano baina yake na wadau na wananchi mbalimbali wanaofanya kazi na Ofisi hii kwa kuwa kupitia maonesho haya Ofisi yake itaendelea kujitangaza kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Ameeleza kuwa kupitia maonesho ya Nanenane Ofisi yake itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kutoa elimu ya msaada wa sheria na ushauri wa kisheria hususan kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ambao ndio walengwa haswa wa maonesho haya ili kusaidia kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mtulo amesema kuwa kupitia maonesho haya Ofisi yake itaendelea kujitangaza kwa wananchi na wadau wake ili kukuza ufahamu kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa wananchi ambayo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi yake katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake Afisa wa Jeshi la Magereza kutoka Gereza la Isanga Dodoma, ndugu Benard Mabula, amemshukuru Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo kwa kutembelea banda la Magereza na kujionea jinsi Jeshi hilo linavyofanya kazi zake za uzalishaji katika kuongeza tija kwa kuwaongezea ujuzi wananchi hasa wafungwa waliopo katika Magereza mbalimbali nchini.

Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, Wafugaji na Uvuvi "Nanenane" mwaka huu yalianza tarehe 1 Agosti, 2025 na yalihitimishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 8 Agosti 2025 katika viwanja vya Nanenane mkoani Dodoma yakiwa yamebeba kauli mbiu isemayo "*Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025.*"



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipatiwa maelezo kuhusu bidhaa mbalimbali zinazopatikana ndani ya Banda la Magereza alipotembelea banda hilo wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapokea Kompyuta Mpakato 30

*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (kushoto) akipokea kompyuta mpakato 30 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndugu Mohammed Khamis Abdulla kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo makabidhiano hayo yalifanyika Wizarani, Mtumba, Dodoma.*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndugu Mohammed Khamis Abdulla, amekabidhi kompyuta mpakato (laptop) 30 kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi, katika hafla fupi iliyofanyika tarehe Agosti 27, 2025, katika ukumbi wa Wizara hiyo uliopo Mji wa Serikali, Mtumba – Dodoma.

Akizungumza kabla ya makabidhiano hayo, Katibu Mkuu ndugu Abdulla alisema Wizara kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali imekabidhi vifaa hivyo vya TEHAMA ili kusaidia na kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wake, Dkt. Possi aliishukuru Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa msaada huo, akibainisha kuwa vifaa hivyo vinakwenda kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa kiwango kikubwa hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa lipo katika mageuzi makubwa kwenye uchumi wa Kidijitali.

"Sisi Mawakili wa Serikali, shughuli zetu nyingi kwa takribani asilimia 90 zinafanyika mahakamani na zinategemea matumizi ya kompyuta. Hivyo, hatua hii ya kutukabidhi vifaa hivi ni wakati muafaka na inaendana moja kwa moja na shughuli



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (kulia) akifurahia kupokea kompyuta mpakato 30 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndugu Mohammed Khamis Abdulla kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo makabidhiano hayo yalifanyika Wizarani, Mtumba, Dodoma.*

zetu za kila siku," alisema Dkt. Possi.

Vilevile, Dkt. Possi aliipongeza Wizara kwa kuendelea kuwezesha mageuzi ya kidijitali nchini, ikiwemo kuhakikisha kunakuwa na gharama nafuu za huduma za intaneti kwa wananchi na taasisi.

Naye, Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Mifumo na Huduma za TEHAMA wa Wizara hiyo, Mohammed Mashaka alisema kuwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali, Serikali inaendelea kugawa vifaa vya TEHAMA kwa taasisi mbalimbali ili kurahisisha huduma, kuziunganisha taasisi hizo ili kuhakikisha huduma na rasilimali muhimu za kidijitali zinapatikana.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyeketi kushoto) akioneshwa kompyuta mpakato na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndugu Mohammed Khamis Abdulla kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye hafla ya makabidhiano ya kompyuta hizo iliyofanyika kwenye ukumbi wa Wizara hiyo, Mtumba, Dodoma.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyeketi mbele kulia) akiwa kwenye kikao na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti na watumishi wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kupokea kompyuta mpakato 30 kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, ndugu Mohammed Khamis Abdulla kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Ofisi hiyo kwenye hafla iliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Wizara hiyo, Mtumba, Dodoma.*




*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Salehe Manoro akitoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi waliotembelea banda la Ofisi hiyo wakati wa kilele cha Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawafikia Wananchi 826 Maonesho ya Nanenane

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupitia zoezi la kutoa elimu ya msaada wa kisheria imefanikiwa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi 826 kutoka maeneo mbalimbali waliofika katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi "NaneNane" yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Utoaji wa huduma hizo umesaidia wananchi kutatua kero na kupata haki zao za msingi kwa njia ya sheria kupitia mikataba mbalimbali, elimu ya uraia, katiba, masuala ya uchaguzi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi.

Huduma nyingine zilizotolewa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho hayo ni kuwajengea uelewa wananchi wanaotembelea banda hilo kuhusu masuala ya kisheria ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi ikiwemo masuala ya mirathi, ardhi, ajira, ndoa, ukatili wa kijinsia, haki madai na jinai.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitumia Maonesho hayo kuwajengea uelewa wadau na wananchi waliofika bandani hapo kuhusu jukumu kuu la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ambalo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi yanayofunguliwa na/dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Akizungumza mmoja wa wananchi waliotembelea banda la Ofisi hiyo ambaye

michango yake ya hifadhi ya jamii ilikuwa haiwasiliwashwi na muajiri wake kwa kipindi cha miaka sita alichofanya kazi kwenye kampuni hiyo.

Aidha, aliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushughulikia suala hilo ambapo Wakili wa Serikali Mwandamizi, Bi. Hosana Mgeni aliwasiliana na muajiri huyo kwa njia ya simu ambaye alikiri kutambua suala hilo na kumtaka mwananchi huyo kufika Ofisini kwake mara moja kwa ajili ya kutatuliwa suala lake.

Akizungumza katika kilele cha Maonesho na Sherehe za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi (Nanenane) zilizofanyika kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema miradi ya umwagiliaji iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa inapaswa kusimamiwa kwa viwango bora ili kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji na kukuza tija ya mavuno.

Aidha, Mhe. Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza bajeti ya kilimo ili kugharamia ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji, mabwawa na visima, pamoja na kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja, huku upatikanaji wa mbegu bora na mbolea ya kisasa ukiimarika kupitia ruzuku na kuanzishwa kwa viwanda vya uzalishaji, hatua iliyoongeza matumizi ya pembejeo nchini.

Ameongeza kuwa ongezeko hilo la bajeti limewezesha miradi ya kimkakati chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Tatu (ASDP III), huku Serikali ikiimarisha huduma ya zana za kilimo na kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea, sambamba na kuhimiza elimu ya matumizi sahihi kwa wakulima.

Katika hatua nyingine, Mhe. Rais Dkt. Samia amezindua Maabara Kuu ya Kilimo yenye viwango vya kimataifa, itakayokuwa kitovu cha maabara zote za kilimo nchini. Maabara hiyo inajumuisha maabara ndogondogo 15 zenye uwezo wa kufanya uchunguzi wa mimea, wadudu, udongo, sumu kuvu, afya ya mimea na kuzalisha miche isiyo na magonjwa pamoja na kuboresha ubora

Mhe. Rais Dkt. Samia ameitaka maabara hiyo kujikita katika kazi za kisayansi na utafiti kwa umakini mkubwa, kwa kuzingatia kwamba jukumu hilo ndilo msingi wa usalama wa chakula wa Taifa, sambamba na kuagiza uanzishaji wa maabara maalum ya utafiti wa mbegu za asili, akisema hifadhi na utafiti wa mbegu hizo ni suala nyeti kwa mustakabali wa kilimo nchini.

Mhe. Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ni nguzo za mageuzi ya uchumi wa Taifa kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo 2050 na Ajenda 10/30 na kuahidi kuendelea kuwekeza, kuwasikiliza wadau na kutumia TEHAMA ili kuongeza ushindani katika sekta hizo.

Akirejea kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane ya mwaka huu, "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025", Mhe. Rais Dkt. Samia aliwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya tarehe 29 Oktoba, 2025 ili kushiriki Uchaguzi Mkuu na kusisitiza kuwa kuchagua viongozi bora ni nguzo ya maendeleo ya Taifa.



*Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hosana Mgeni akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bunge na Msalato kuhusu masomo ya kuzingatia ili kuwa Wakili wa Serikali walipotembelea Banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Kilele cha Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



# Watumishi wa Serikali Wahimizwa Kupima Afya Zao

*Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Biteko akifungua mashindano ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akiwa kwenye picha ya pamoja na wachezaji wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kuanza maandamano ya ufunguzi wa Mashindano ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza.*

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko, ametoa rai kwa watumishi wa Umma wanaoshiriki michezo ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) kupima afya zao kabla ya kuanza kushiriki mashindano hayo ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza wakati wa mashindano hayo.

Mhe. Dkt. Biteko alitoa rai hiyo tarehe 7 Septemba 2025, wakati akifungua mashindano ya 39 ya SHIMIWI yaliyofanyika

katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo hayo, Mhe. Dkt. Dotto Biteko amewataka watumishi hao kufanya vipimo mbalimbali ikiwemo moyo na shinikizo la damu ili kuhakikisha kila mtumishi anayeshiriki michezo hiyo anakuwa imara wakati wote wa mashindano hayo.

Mhe. Dkt. Biteko amewataka wanamichezo kufanya mazoezi mara kwa mara ikiwemo mazoezi ya awali kwa ajili ya kupasha moto misuli kabla ya kuanza mchezo husika ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kujenga utimamu na uimara wa mwili wakati wote wa mashindano.

Aidha, kiongozi huyo aliwataka watumishi hao kujiandaa kiakili na kifikra wakati wote wa mchezo ili kumkabili mpinzani kwa lengo la kuhakikisha timu inafikia malengo iliyojiwekea kwa kuwa wataalamu husema mafanikio huanzia katika fikra ya mchezaji.

Mhe. Dkt. Biteko pia amewapongeza waajiri walioruhusu watumishi wao kushiriki mashindano hayo huku akitoa rai kwa waajiri ambao hawakuruhusu watumishi wao kushiriki mashindano hayo mwaka huu, kuhakikisha wanashiriki mashindano hayo mwakani ikiwa ni kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, sanjari na kuongeza idadi ya watumishi wanaoshiriki SHIMIWI.

Naibu Waziri Mkuu, Mhe. Dkt. Dotto Biteko amewataka waratibu wa mashindano hayo kuwekeza kwenye michezo kwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa, tasnia ya michezo na burudani Tanzania, imeendelea kukua kwa kasi na kuchangia sehemu muhimu na kubwa katika kukuza pato la Taifa na kuongeza ajira nchini hatua ambayo imesaidia wananchi wa rika zote kujiletea maendeleo.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akimsikiliza Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Biteko wakati akifungua mashindano ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza.*

akizungumza mara baada ya ufunguzi wa Mashindano hayo ameipongeza timu ya kuvuta Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kufanikiwa kuingia hatua ya robo fainali baada ya kuivuta timu ya kuvuta kamba ya wanawake wa Wizara ya Viwanda.

Aliwataka wachezaji hao kujipanga vyema na kufuata maelekezo ya mwalimu ili waweze kufanya vizuri katika michezo inayofuata ili kuhakikisha wanaendelea kupeperusha vyema bendera ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika mashindano hayo.

Kiongozi huyo ameendelea kuwatia moyo wachezaji wa timu ya wanaume wa mpira wa miguu na kamba baada ya kutolewa katika mashindano hayo, kutokata tamaa huku akiwataka kujipanga vizuri katika mashindano yajayo ili waweze kufanya vizuri zaidi.

Mashindano ya Michezo ya 39 ya SHIMIWI kwa mwaka 2025 yalihitimishwa Septemba 16, 2025, ambayo yaliyoongozwa na kaulimbiu isemayo, "Michezo kwa Watumishi Huongeza Tija Kazini, Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa Amani na Utulivu".



*Wachezaji wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Biteko wakati akifungua mashindano ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza.*



*Wachezaji wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Biteko wakati akifungua mashindano ya Shirikisho la michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika Jijini Mwanza.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akikabidhi funguo ya gari kwa Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mkoa wa Manyara ndugu Lameck Butuntu katika makabidhiano yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Manyara Yakabidhiwa Gari

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Manyara imefanikiwa kupata gari mpya ambayo itasaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku kwa wakati.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi gari hiyo aina ya Toyota Hilux Jijini Dodoma, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo amesema kuwa uwepo wa gari hiyo utasaidia utekelezaji wa majukumu ya kila siku hatua itakayosaidia kuongeza tija, ufanisi na kuleta matokeo chanya yatakayosaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Manyara kufikia malengo iliyojiwekea kwa wakati.

Aliongeza kuwa uwepo wa gari hiyo ni jitihada za Ofisi Wakili Mkuu wa Serikali kuboresha mazingira ya utendaji kazi hasa ukizingatia jiografia ya Mkoa huo ambapo Mawakili wamekuwa wakitumia muda mrefu kutoa huduma kutokana na umbali uliopo kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine.

Kwa upande wake Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Manyara ndugu Lameck Butuntu ameishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia gari hiyo huku akifafanua kuwa gari hiyo itasaidia

kupunguza changamoto za kiutendaji zilizokuwepo kwa kuwa sasa wataweza kutekeleza majukumu yao kwa wakati ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo ikiwemo yale maeneo yaliyokuwa hayafikiki kwa wakati.

Alieleza kuwa ujio wa gari hiyo utasaidia kutembelea wilaya, tarafa, kata za mkoa huo kwa wakati ili kuhakikisha wanaisaidia Serikali na wananchi kupata haki zao kwa kuwa gari hiyo itawasadia kutembelea maeneo yenye migogoro hatua itakayosaidia kuendesha na kumaliza mashauri hayo kwa wakati.

Akielezea faida zitakazopatikana kutokana na ujio wa gari hilo, Ndugu Butuntu alisema kuwa Mawakili wa Serikali mkoani humo sasa watafika mahakamani kwa wakati tofauti na awali ambapo iliwalazimu kuazima magari kutoka taasisi nyingine za Serikali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.


Aidha, Ndugu Butuntu alisema kuwa gari hiyo itasaidia kuongeza tija hasa katika ubebaji na usambaji wa nyaraka mbalimbali kwa kuwa sasa nyaraka zote za Ofisi zitasambazwa kwa usalama na ufanisi zaidi na hivyo kuondoa uwezekano wa kuchelewa au kupotea kwa nyaraka za mashauri ya Madai na usuluhishi yanayoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo.

Ndugu Butuntu alisema kuwa uwepo wa gari hilo utawasaidia sana Mawakili kuendesha Mashauri kwa wakati hasa pale wanapokuwa na shauri zaidi ya moja katika mahakama tofauti mkoani humo ikiwa ni pamoja na kushiriki mashauri mbalimbali na kutembelea maeneo yote yenye migogoro ili kuona uhalisia wa mashauri wakati wa kukusanya ushahidi hasa katika mashauri yanayohusu migogoro ya aridhi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Manyara, inahudumia jumla ya Wilaya tano za Mkoa huo ambazo ni Wilaya ya Babati, Mbulu, Hanang', Kiteto na Simanjiro.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akikata utepe kabla ya kukabidhi gari kwa Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mkoa wa Manyara ndugu Lameck Butuntu katika makabidhiano yaliyofanyika Jijini Dodoma. Anayeshuhudia kushoto ni Wakili wa Serikali Mfawidhi Mkoa wa Manyara Ndugu. Lameck Butuntu.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akipeana mkono na Wakili wa Serikali Mfawidhi Mkoa wa Manyara, Ndugu. Lameck Butuntu mara baada ya kukabidhi gari hiyo Jijini Dodoma.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa tatu kutoka kushoto) akiwa pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Manyara mara baada ya kukabidhi gari hiyo Jijini Dodoma. Wa Pili kushoto ni Mkurugenzi wa Idara ya Madai ndugu Mark Mulwambo wa Ofisi hiyo.*



# Zingatieni Sheria, Taratibu na Kanuni za Manunuzi

*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Wakuu wa Idara na Vitengo wakati akifungua Kikao Kazi cha Maandalizi ya Mpango wa Ununuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 kilichofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

Wakuu wa Idara na Vitengo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametakiwa kufanya ununuzi wa mahitaji wanayotarajia kununua kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 kwa kufuata Mpango wa Ununuzi wa Ofisi hiyo ili kupunguza migongano ya kimanunuzi ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Wito huo ulitolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo wakati akifungua kikao kazi kuhusu Maandalizi ya Mpango wa Ununuzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 kilichofanyika kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza na viongozi hao Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo amesema kuwa uwepo wa Mpango wa Ununuzi ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni takwa la kisheria ambalo inaitaka kila taasisi ya umma kuwa na Mpango wa Ununuzi kwa kila Mwaka wa Fedha husika.

“Sheria ya Ununuzi wa Umma inazitaka taasisi zote za umma kuwa na mpango wa ununuzi wa kila Mwaka wa Fedha husika.” Alisema Bi. Mtulo.

Bi. Mtulo ameongeza kuwa Mpango huu utasaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuonyesha mahitaji halisi ya taasisi kwa mwaka mzima ambao utatumika kama

kama msingi wa uidhinishaji wa zabuni na manunuzi zinazotarajiwa kutangazwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

Kiongozi huyo ameeleza kuwa kama Mpango wa Manunuzi Utasimamiwa vizuri utasaidia kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika nyanja mbalimbali ikiwemo ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ili kuongeza tija katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa njia ya mtandao.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi Serikalini Bi. Hellen Lubogo amesema kuwa uwepo wa Mpango wa ununuzi utaisaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupanga bajeti yake kwa ufanisi kwa kuoanisha mahitaji halisi na fedha zilizotengwa kwa mwaka husika hatua itakayopunguza matumizi ambayo hayakupangwa, kurudia manunuzi, na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma ndani ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

Aidha, Bi. Lubogo amesisitiza kuwa Mpango wa Ununuzi ni nyenzo muhimu inayosaidia kuweka uwazi kwa wadau wa ndani na nje ya taasisi ikiwa ni pamoja na kuonyesha vipaumbele vya taasisi na namna fedha za umma zitakavyotumika, hivyo kuongeza uwajibikaji wa Menejimenti ya OWMS.

Mpango wa Ununuzi wa Mwaka wa Fedha 2025/26 wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni chombo muhimu kitakachosaidia kuhakikisha uwajibikaji, ufanisi, ubora wa huduma, na matumizi bora ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria na miongozo ya ununuzi serikalini.



*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Hellen Lubogo akitoa neno la utangulizi wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya Mpango wa Manunuzi kilichofanyika Kibaha mkoani Pwani.*





*Mhasibu Mwandamizi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Nengai Samweli akiwasilisha Mpango wa Manunuzi wa Kitengo cha Uhasibu na Fedha wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya Mpango wa Manunuzi kilichofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yasogeza Huduma Karibu na Wananchi

*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Mhe. Devota Kamuzora alipofika mahakamani hapo wakati wa ziara yake katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Manyara.*

Mahakama ya Tanzania imeipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kufungua Ofisi kwenye mkoa wa Manyara ili kusogeza huduma karibu na wadau na wananchi ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake

Hayo yameelezwa na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Masijala Ndogo ya Manyara, Mhe. Devotha Kamuzora wakati wa ziara ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofika mahakamani hapo.

Mhe. Jaji Kamuzora amesema kuwa ufunguzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye mkoa huo ni jambo zuri kwa kuwa wamesogeza huduma karibu na wadau na wananchi wanaowahudumia kwa kuwa hapo awali Mawakili wa Serikali wa Ofisi hiyo walikuwa wanatoka mkoa wa Arusha kuja Manyara kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali na taasisi zake hivyo kupelekea ucheleweshaji wa usikilizaji wa mashauri hayo.

“Ufunguzi wa Ofisi Manyara umerahisisha na kuharakisha uendeshaji wa mashauri kwa kuwa Mahakama kuu Kanda ya Manyara tumejiwekea malengo ya kuendesha na kumaliza shauri kwa muda usiozidi miezi sita. Hivyo, ziara yako ya kutembelea Ofisi inakupa picha halisi na kuboresha mazingira ya kazi ili Mawakili waweze kuwahudumia vizuri wadau,”

alifafanua Mhe. Jaji Kamuzora.

Bi. Mtulo alisema kuwa lengo la ziara yake ni kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo na kujua changamoto wanazokabiliana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kama Mawakili wa Serikali. Aidha, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mtulo alishuhudia namna Ofisi ya Mkoa huo inavyoendesha mashauri kwa wakati kwa kushirikiana na Mahakama na Mawakili wengine wa taasisi za Serikali.

Naye Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Mhe. Bernard Mpepo amewapongeza Mawakili wa Serikali wa Mkoa wa Manyara wanaofanya kazi na Mahakama hiyo kwa kutoa ushirikiano kwa Majaji na Mawakili wengine wa taasisi za Serikali kuendesha mashauri ya Serikali na kusogeza huduma karibu na wananchi wa mkoa wa Manyara.



*Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Mhe. Devotha Kamuzora akizungumza na Ujumbe wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ukiongozwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Manyara.*



*Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Lameck Butuntu akimtambulisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo na ujumbe wake walipofika Mahakama Kuu Kanda ya Manyara kukagua utendaji wa Ofisi hiyo.*



*Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Mhe. Bernard Mpepo akizungumza na Ujumbe wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ukiongozwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (hayupo pichani) akiwa ziarani mkoani humo.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa pili kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Mhe. Devotha Kamuzora (aliyesimama katikati) baada ya kikao cha ukaguzi wa utendaji kazi wa Ofisi hiyo mkoani humo.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akimsikiliza na kujadiliana jambo na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Mhe. Dkt. Frank Mirindo alipofika mahakamani hapo wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Mawakili wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani humo.*

# OWMS Yapunguza Gharama Kwa Wadau ya Kupata Ushauri wa Kisheria

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) yapunguza gharama za kupata ushauri mbali mbali wa kisheria kwa wadau ambao wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kutoka mkoa wa Tabora kwenda mikoa ya jirani kupata ushauri wa kisheria.

Hayo yameelezwa na Kaimu Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Tabora, ndugu Gureni Mapande wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofanya ziara ya kukagua utendaji kazi wa Mawakili wa Serikali wa Ofisi hiyo mkoani Tabora.

Mapande alisema kuwa, “OWMS Tabora imefanikiwa kusogeza huduma karibu na wananchi mathalani mdau anayekusudia kuishtaki Serikali hatumii gharama za kusafiri kwenda mikoa mingine kupeleka notisi ya kusudio la kuishtaki Serikali bali notisi hiyo inawasilishwa na OWMS Tabora.”

Akiwa ziarani mkoani humo Bi. Mtulo alisema kuwa lengo la ziara yake ni kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo kwenye mikoa mbali mbali ikiwemo mkoa wa Tabora ikiwemo namna Mawakili wa Serikali wa Ofisi hiyo wanavyoendesha mashauri kwa niaba ya Serikali, ushirikiano wa Mawakili hao na wadau wa OWMS ikiwemo mahakama, halmashauri mbali mbali na taasisi nyingine za Serikali ili OWMS iweze kubaini uhalisia, kupata changamoto, kuona mazingira ya utendaji kazi, kupata maoni na kuyafanyia kazi ili kuboresha utendaji

kazi wa OWMS.

Pia, Bi. Mtulo alikutana na Mawakili wa Serikali wa Halmashauri za Mkoa wa Tabora na kutoa rai kwao ya kuhakikisha wanashiriki vikao na majukumu yao yanayohusu masuala ya kisheria yanayotekelezwa kwenye halmashauri zao na wawasilishe changamoto wanazokutana nazo kwa viongozi wa maeneo yao na kwa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Ofisi za Mikoa hususan changamoto zinazohusu uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili yaweze kufanyiwa kazi kwa wakati.

Aidha, Bi. Mtulo aliwaeleza Mawakili wa Serikali wa Halmashauri hizo kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imewapa kibali Mawakili wa taasisi za Serikali waliopo kwenye halmashauri zote nchini kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali hivyo watumie vibali walivyopewa kuendesha mashauri hayo kwenye maeneo yao.

Naye Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Mhe. Dkt. Frank Mirindo amempongeza Bi. Mtulo kwa kufanya ziara ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo kwenye mkoa wa Tabora na amemweleza kuwa Mawakili wa Ofisi hiyo wanafika mahakamani kwa wakati na kuendesha mashauri vizuri kwa niaba ya Serikali



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa kwanza kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Mhe. Dkt. Frank Mirindo (aliyesimama katikati) alipofika Mahakamani hapo kufuatilia utendaji kazi wa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yake mkoani Tabora.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akisaini kitabu cha wageni alipofika kwenye Mahakama Kuu Kanda ya Tabora kufuatilia utendaji kazi wa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yake mkoani Tabora.*



*Kaimu Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Tabora, ndugu Gureni Mapande akizungumza na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofika mkoani humo kukagua utendaji kazi wa Ofisi hiyo.*




# Serikali Yaahidi Sheria Rafiki Kwa Wawekezaji Kufanikisha Dira 2050

*Msajili wa Hazina, ndugu Nehemiah Mchechu akizungumza wakati wa kikao kazi baina ya Ofisi yake na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kilichofanyika Kibaha, Pwani.*

Serikali imeeleza dhamira yake ya kutengeneza sheria rafiki za uwekezaji zitakazoiwezesha kufikia uchumi wa kati na wa juu kama ilivyobainishwa kwenye Dira 2050.

Moja ya shabaha za Dira 2050 ni kuchochea ukuaji wa Pato la Taifa kutoka pato la $80 billioni ya sasa mpaka $1trilioni ifikapo mwaka 2050. Kufikia lengo hilo, Serikali imesema ni lazima iendelea kutengeneza mazingira mazuri ya biashara yatakayowezesha taasisi za umma kufanya vizuri kwa kushirikiana na sekta binafsi.
Hayo yalisemwa Oktoba 16, 2025 wakati wa kikao kazi kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kilichofanyika Kibaha, mkoani Pwani.

Msajili wa Hazina, ndugu Nehemiah Mchechu alisema maagizo waliyopewa na Mhe. Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni uboreshwaji wa sheria ili ziendane na maono yaliyomo kwenye Dira 2050.
"Tunapaswa kuwa na sheria ambazo zitaongeza ufanisi wa taasisi za umma. Tunapaswa

kuwa na sheria ambazo zitatoa wigo kwa sekta za umma kufanya kazi kwa ukaribu na sekta binafsi," alisema ndugu Mchechu. Alisema kuongezeka kwa ufanisi wa sekta za umma, kutapelekea ongezeko la mchango wake kwenye mapato ya ndani ya serikali kutoka asilimia nne ya sasa mpaka kufikia kumi miaka minne ijayo, kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Tunapaswa kuboresha huduma na bidhaa zetu, pamoja na kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima ili kuongeza mapato na hatimaye gawio kwa Serikali," alisisitiza ndugu Mchechu. Serikali inataka kuona tija katika uwekezaji wake wa shilingi trilioni 92.3 ilioufanya katika taasisi za umma na kampuni ambazo ina umiliki wa hisa chache.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel Maneno alisema kuwa uimara wa taasisi za umma na sekta binafsi unategemea ubora wa sheria zinazosimamia uwekezaji. Alieleza kuwa usimamizi wa mikataba ya uwekezaji usipokuwa mzuri, itakuwa ngumu au itachukua muda mrefu kufikia matarajio yaliyowekwa na Serikali.

"Aidha, hali hii inaweza kuibua migogoro na hivyo kupelekea kuwakatisha tamaa wawekezaji," alisema ndugu Maneno huku akibainisha kuwa Serikali haiko tayari kufikia hatua hiyo. "Eneo hili la usimamizi wa mikataba tunalipa kipaumbele kikubwa.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akichangia mada wakati wa kikao kazi baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi yake na wadau wengine kuhusu sheria rafiki za kufanikisha utekelezaji wa Dira 2050 kilichofanyika Kibaha, Pwani.*

Kwa mwaka mmoja wa fedha tunaweza kusimamia kati ya mitaba 15,000 na 20,000.

"Na ili kufanya usimamizi wa mikataba hii uwe wa ufanisi, tumeona haja ya kukumbatia matumizi ya teknolojia ili kurahisisha ufuatiliaji." Aidha, alielezea haja ya kuepuka urasimu usiokuwa wa lazima ili wawekezaji, hasa katika eneo la ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Kwa upande wake Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi, alisema sheria za nchi hazitakiwi ziwe kikwazo kwa wawekezaji, badala yake ziwe kivutio. "Ili ndoto yetu ya kuwa na uchumi unaofikia dola za marekani trilioni moja (1$ trillion) ifikie, tunapaswa kuendelea kutengeneza mazingira rafiki ya biashara yatakayovutia wawekezaji zaidi," alisema. Sanjari na hilo, Dkt. Possi alisema nchi inapaswa kuendelea kuboresha usimamizi wa mikataba, hususan katika eneo la PPP. Aidha, alisema taasisi za umma zina jukumu la kutoa gawio na kukuza uchumi wa nchi. "Lakini hili haliwezi kutimia ikiwa taasisi

hizo zitagubikwa na mashauri ambayo yatazilazimu kulipa fedha baada ya hukumu ya mahakama kutolewa na ni katika muktadha huo tumekutana kujadili namna bora ya kukabiliana na mapungufu ya kisheria," alihitimisha Dkt. Possi.

Naye Mwandishi Mkuu wa Sheria, ndugu Onorius Njole alisema kufikia uchumi wa dola za marekani trilioni moja (1$ trillion) unategemea uimara wa taasisi za umma na ndio maana ipo haja ya kuwa na mfumo imara wa kisheria katika eneo la uwekezaji. "Ni lazima mashirika ya umma yasimamiwe na sheria za uwekezaji ambazo zinaendana na mahitaji ya sasa," alisema.

"Mfumo wa sheria lazima uendane na kasi ya ukuaji wa uwekezaji katika mashirika ya umma."




*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndugu Samwel Maneno akichangia mada wakati wa kikao kazi kuhusu sheria rafiki za kufanikisha utekelezaji wa Dira 2050 kilichofanyika Kibaha, Pwani.*




*Mwandishi Mkuu wa Sheria, ndugu Onorius Njole akizungumza wakati wa kikao kazi kuhusu sheria rafiki za kufanikisha utekelezaji wa Dira 2050 kilichofanyika Kibaha, Pwani.*







*Baadhi ya wajumbe wa kikao kazi kuhusu sheria rafiki za kufanikisha utekelezaji wa Dira 2050 wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) akizungumza kwenye kikao hicho kilichofanyika Kibaha, Pwani*




*Wachezaji wa timu ya mpira wa miguu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakipasha misuli moto kabla ya kuanza kwa mchezo dhidi ya timu ya mpira wa miguu ya Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Mabatini Jijini Mwanza.*

# Wakili Mkuu Sports Club Yaibagaza Osha Sports Club

Timu ya Mpira wa Miguu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Wakili Mkuu Sports Club), imefanikiwa kuiduwaza timu ya mpira wa miguu ya Wakala wa Serikali Mahala pa Kazi (OSHA) baada ya kibuka na ushindi wa bao 1-0 Katika mchezo uliochezwa kwenye uwanja wa shule ya Msingi Mabatini jijini Mwanza.

Katika mchezo huo ulioanza majira ya saa 4.00 asubuhi, timu ya Wakili Mkuu wa Serikali iliuanza mchezo huo kwa kasi hali iliyopelekea kufanya mashambulizi mengi ya hatari langoni mwa timu ya OSHA.

Timu ya mpira wa miguu ya Wakili Mkuu Sports Club, walisubiri mpaka dakika ya 17 ya kipindi cha kwanza baada ya mpira mrefu uliopigwa na mlinda mlango machachali ndugu Ditrick Luambano na kumkuta kiungo hatari wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Joseph Bundala aliyetuliza mpira huo kwa ustadi wa hali ya juu na kutoa pasi maridhawa kwa ndugu Egidy Mkolwe ambaye hakufanya ajizi na kuukwamisha mpira huo wavuni.

Kupatikana kwa bao hilo kuliamsha furaha, nderemo, hoi hoi na vifijo kwa mashabiki wa timu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao waliendelea kuimba nyimbo mbalimbali zenye lengo la kuhanikiza ushindi wa timu yao mpaka timu hizo zilipoenda mapumziko ya kipindi cha kwanza cha mchezo huo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa mbele kwa goli 1- 0.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi ambapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, iliendelea kulisakama lango la mpinzani wake bila huruma wakati wote wa mchezo kwa kupiga mashuti mengi langoni ambayo mengi yalitoka nje ya uwanja.

Baada ya kufanya mashambulizi mengi bila mafanikio nusura timu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iandike bao la pili

kufuatia shuti kali lililopigwa na mshambuliaji hatari wa timu hiyo ndugu Habibu Rajabu lililogonga mwamba na kutoka nje.

Akizungumza baada ya mchezo huo kocha wa timu ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Denis Lipiki amewapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi huo ambao umesaidia kuongeza ari ya kufanya vizuri kwenye michezo ijayo.

Ameongeza kuwa ushindi uliopatikana leo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na moyo wa kujitolea wa wachezaji hao pamoja na kufuata maelekezo ambayo amekuwa akiwapa yaliyopelekea wachezaji wake kucheza kama timu na kuelewana vyema wakati wote wa mchezo na kufanikiwa kupata ushindi huo.

Kwa upande wake nahodha wa timu hiyo, ambaye ndiye mfungaji wa bao pekee liloipatia ushindi timu ya Wakili Mkili Mkuu wa Serikali, Ndugu Mkolwe amewapongeza wachezaji kwa ushindi wa leo huku akitoa rai kwa timu pinzani kujiandaa kupokea pumzi ya moto katika mechi zinazofuata.

Aidha, ametumia nafasi hiyo kuushukuru uongozi na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wanaoipa timu yake ikiwa ni pamoja na kusaidia kupata kambi nzuri, mwalimu mwenye weledi wa hali ya juu ambaye amekuwa chachu ya timu hiyo kufanya vizuri.

Aidha, timu ya Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya vizuri baada ya kuwavuta timu ya Kamba ya Wanawake wa Wizara ya Viwanda, bila huruma hatua ambayo imeongeza morali ya timu hiyo kuendelea kufanya vizuri katika michezo inayofuata.

Timu ya mpira wa miguu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepangwa kundi E lenye timu za Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Kilimo, OSHA na Wizara ya Madini, imeingia mawindoni kujinoa na mchezo unaofuata dhidi ya timu ya Mahakama ya Tanzania, katika mchezo unaotarajiwa kuchezwa kwenye uwanja wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru iliyopo Jijini Mwanza.



*Wachezaji wa timu ya Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakivuta Kamba dhidi ya timu ya Wanawake wa Wizara ya Viwanda katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza.*



*Wachezaji wa timu ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakivuta Kamba dhidi ya timu ya Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza.*

# Timu ya Kamba ya Wanawake Yaibuka Kidedea

Timu ya wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu Wa Serikali, ilifanikiwa kuibuka mshindi baada ya kupata alama moja kati ya alama mbili zinazotakiwa katika mzunguko wa kwanza wa mchezo wa kuvuta kamba wakati wa mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) iliiyofanyika jijini Mwanza.

Michuano hiyo iliyoanza tarehe 1 Septemba 2025 katika viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza, timu ya kuvuta kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipata ushindi huo kwa kuwavuta timu ya wanawake wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, ikiwa ni mchezo wa kwanza wa kundi H uliozikutanisha timu hizo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo Nahodha wa timu hiyo Bi. Magreth Lihawala amesema kuwa mafanikio hayo yaliyopatikana yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na maandalizi mazuri yaliyofanywa na timu hiyo ikiwa ni pamoja na kuzingatia maelekezo na mbinu za Mwalimu ndugu Denis Lipiki muda wote wa mazoezi.

Bi. Lihawala ameeleza kuwa, licha ya ugumu na uzoefu wa timu waliyocheza nayo, amewapongeza wachezaji wake kwa moyo wa kujituma na kupambana, wakati wote wa mchezo huo hasa katika mzunguko wa kwanza ambapo ndipo walipofanikiwa kupata ushindi huo kwa kuwavuta timu ya wanawake kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Aidha, Nahodha wa timu

hiyo, Bi. Lihawala ameeleza kuwa, mpango uliopo katika michezo inayofata ni kuongeza umakini, jitihada na kufuata maelekezo ya mwalimu ili kuhakikisha wanashinda michezo ya mizunguko yote miwili hatua itakayosaidia timu hiyo kusonga mbele na kuibuka kidedea mwisho wa mashindano hayo.

Kwa upande wa timu ya Kamba ya Wanaume wa Ofisi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametoka suluhu mchezo wa mzunguko wa kwanza na kupoteza katika mzunguko wa pili wa mchezo huo huku timu ya mpira wa miguu wanaume wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikikubali kipigo cha goli moja bila majibu dhidi ya timu ya Wizara ya Kilimo.

Michuano ya SHIMIWI iiyoanza tarehe 1 Septemba, 2025 inategemewa kuhitimishwa tarehe 16 Septemba 2025 huku zaidi ya timu 70 zikitarajiwa kushiriki michezo mbalimbali ambayo ni mpira wa miguu, kuvuta kamba, mpira wa pete, karata, bao, drafti na riadha.




*Wachezaji wa timu ya Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakiwa kwenye picha ya pamoja kabla ya kuchuana vikali na timu ya kamba ya wanawake wa Ofisi ya Waziri Mkuu  Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi Ampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Dkt. Ally Possi**
Wakili Mkuu wa Serikali

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amempongeza Mhe. Hamza Said Johari kwa kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassankuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Dkt. Possi amesema kuwa uteuzi huu umetokana na umahiri wake katika kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali, kufanya kazi bila kuchoka na kuwa tayari kusimamia masuala ya kisheria kwa kuzingatia Katiba, usawa na haki ili kuimarisha misingi ya utawala wa sheria na utawala bora kwa lengo la kuendelea kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, Dkt. Possi amemtakia kheri na mafanikio Mhe. Hamza Johari katika utekelezaji wa majukumu yake, na kutumia fursa hiyo kuendeleza ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na ofisi zote zilizopo kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini ili kutekeleza kwa vitendo dhana ya utoaji haki nchini kuendana na dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2050.

Akizungumza mara baada ya kuwasili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Johari alimshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuendelea na majukumu ya kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria.

"Nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu na kuniteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuendelea kuishauri Serikali kama ilivyoainishwa katika Katiba na Sheria, Namshukuru sana Mhe. Rais." Amesema Mhe. Hamza Johari

Mhe. Johari ametumia fursa hiyo kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wote waliopo kwenye

mnyororo wa utoaji haki na kuwataka waendelee kufanya kazi kwa bidii na kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kiongozi huyo amewataka Watumishi hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuboresha fikra zao ili waendelee kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwa Mhe. Rais amewaamini ili waweze kumsaidia majukumu kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Akitoa salamu za pongezi Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bw. Eliakimu Maswi, amempongeza Mhe. Hamza S. Johari kwa kuteuliwa na kuapishwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Eliakimu Maswi ameendelea kumpongeza Mhe. Johari kwa heshima aliyopewa, kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hiyo na kuahidi kumpa ushirikiano wakati wote kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hizo.



## HOTUBA YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN WAKATI WA KUAPISHWA KUWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, TAREHE 3 NOVEMBA, 2025 - CHAMWINO, DODOMA

***Habari ya asubuhi.***

Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku uhai na kutuwezesha kushiriki sherehe hizi za kihistoria kwa Taifa letu. Pili niwashukuru Watanzania wote kwa imani yao kwa Chama cha Mapinduzi, na kwa mapenzi makubwa, na kutupa mimi na Makamu wa Rais fursa hii adhimu ya kuwatumikia.

Shukrani za kipekee kwa Viongozi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi, kwa namna walivyoendesha kampeni kwa mafanikio makubwa.

Niishukuru tena Tume ya Uchaguzi kwa kuratibu na kusimamia mchakato mzima wa uchaguzi kwa ufanisi usiotiliwa shaka.

***Ndugu Viongozi;***

***Ndugu Wananchi;***

Katika Uchaguzi huu tulikuwa na wagombea 17 kutoka vyama mbalimbali vya siasa tukiwania nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kuwashukuru wenzangu 17 ambao kwa hakika mmeonesha ukomavu wa kidemokrasia kwa kuendesha kampeni ambazo tulishindana kwa hoja, na sote tulionesha, kuwa siasa sio vita. Tumemaliza vyema uchaguzi na kumpongeza alieshinda.

Aidha, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi na Vyama vya Siasa vilivyokuwa kwenye mchakato wa uchaguzi, kwa kumaliza uchaguzi kwa salama na amani. Zanzibar Oyeee!

Pongezi zangu pia ziwaendee wote walioshinda kwenye nafasi za Ubunge; Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi; na Udiwani kote nchini. Kwa wote niwaambie uchaguzi umekwisha, sasa tukafanye kazi ya kulijenga Taifa letu, na Utu wa Mtanzania.

***Waheshimiwa Marais;***

***Viongozi;***

***Ndugu Wananchi;***

Shughuli inakuwa nzuri na ya kufurahisha ikihudhuriwa na wanaokupenda. Tanzania leo imejawa na furaha kubwa kuona baadhi ya Waheshimiwa Marais wenzangu na viongozi mbalimbali wa nchi jirani wamejumuika nasi katika tukio hili, pamoja na kwamba tulitoa mwaliko kwa muda mfupi. Kwa wale

walioshindwa kushiriki tunatambua uzito wa majukumu yao, na tunajua mioyo yao ipo pamoja nasi. Tunawashukuru pia wote waliotuma salamu za pongezi kwetu. Tunasema ahsanteni sana.

***Ndugu Wananchi;***

Uchaguzi ni fursa kwa Wananchi kueleza matakwa yao ya aina ya viongozi wanaodhani wataweza kuwatumikia vyema, na kuwaletea maendeleo endelevu. Kipindi cha kampeni tuligawika kiitikadi na kishabiki kama taifa. Ila baada ya uchaguzi kufanyika, anaechaguliwa na wengi huwa ndio chaguo la nchi na anapaswa kuwa Mtumishi wa Wananchi wote, waliomchagua, waliochagua wagombea wengine, na hata ambao hawakushiriki uchaguzi. Kwa sisi tuliochaguliwa, ahadi yetu ni kulitumikia Taifa hili kwa nguvu zetu zote, vipawa vyetu vyote na maarifa yetu yote.

Ndugu zangu Watanzania, ni vyema tutambue kuwa uchaguzi mkuu wa Viongozi wa Serikali ni mchakato wa msimu mmoja tu ndani ya miaka mitano. Muda mwengine wote maisha lazima yaendelee. Hivyo basi, Jukumu letu sote kwa pamoja, ni kujenga nchi yetu na kuifanya kesho yetu iwe bora zaidi kuliko jana yetu. Niwasihi tuendelee kuilinda itikadi yetu ya umoja na mshikamano.

***Ndugu Wananchi;***

Wote tunaoitakia mema nchi hii tumesikitishwa na kuhuzunishwa na matukio ya uvunjifu wa amani, upotevu wa maisha na uharibifu wa mali za Umma na mali za Watu binafsi kwenye baadhi ya maeneo nchini, hasa kwenye Majiji na Miji. Kilichotokea hakiendani na taswira na sifa za Kitanzania na sio Utanzania. Haikutushangaza kuona kuwa baadhi wa vijana waliokamatwa kutokana na kadhia hio wametoka nje ya Tanzania. Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinaendelea kufuatilia na kuchunguza kwa undani zaidi kilichotokea, na kuirudisha nchi katika hali tuliyoizowea kwa haraka. Kamati ya Ulinzi ya Kitaifa, na Kamati za Ulinzi za Mikoa na Wilaya, hakikisheni kuanzia leo maisha ya Wananchi yanarejea mara moja. Pia nitumie fursa hii, kutoa onyo kwa wale wote waliochochea uvunjifu wa amani, na nawataka watambue kuwa vurugu na uvunjifu wa amani huishia kupimana nguvu na uwezo wa kujihami, ila mazungumzo huzaa mshikamano. Tuchague lenye manufaa kwetu, kwani usalama wa Taifa lolote hulindwa na wote kwa nguvu na gharama zozote.

***Ndugu Viongozi;***

***Ndugu Wananchi;***

Kama kawaida, kwa nchi zenye mfumo wa Kidemokrasia hualika waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya za Kimataifa na Kikanda kuja kushuhudia mchakato wa uchaguzi. Uwepo wao huongeza uhalali wa juhudi zetu za kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwenye mazingira ya uwazi, haki, heshima na utawala wa sheria. Kwa muktadha huu, tunazishukuru Jumuiya zote zilizoleta waangalizi wa uchaguzi. Kutoka Afrika tulikuwa na waangalizi kutoka

Umoja wa Afrika (AU); Jumuiya ya nchi za Maziwa Makuu (ICGLR); Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika (SADC); na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Pamoja na hao, tulikuwa na wengine kutoka maeneo mbalimbali. Makundi yote ya waangalizi yameshatoa taarifa za awali, na tunawashukuru kwa kuwa nasi, na kwa heshima kubwa tumepokea maoni yenu. Hata hivyo, kama alivyowahi kusema Rais wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa mwaka 2000 wakati akiapishwa kuwa Rais, na hapa ninakinukuu kipande cha Hotuba hiyo, kinachosema

''nawashukuru watazamaji wa kimataifa kuja kushuhudia uchaguzi wetu ulivyofanyika, walipotusifia tumepokea sifa hizo kwa unyenyekevu. Tumesikia pia waliyodhani hayakwenda sawa na mengine hata sisi tumeyaona. Maagizo yao tumeyakataa, ushauri wao tutauzingatia ili tufanye vizuri zaidi siku zijazo."

***Ndugu Wananchi;***

Sifa moja ya Mwanadamu ni kutokukamilika, aliekamilika kabisa kabisa bila kasoro yoyote ni Mwenyezi Mungu peke yake. Ndio maana, katika shughuli au harakati za wanaadamu tunaunganishwa na mawasiliano, mazungumzo na maelewano, au kwa maneno mengine, tunaunganishwa na uwepo wa Suluhu ya mambo katika jamii zetu. Kama mnavyofahamu, katika kuliunganisha Taifa, Serikali ya awamu ya sita tulianza na falsafa ya 4R's, inayosimamia misingi ya kuzungumza na kuelewana (Reconciliation), kuvumiliana (Resilience), kubadilisha mwelekeo baada ya maelewano (Reforms) na kuendelea kujenga Taifa letu (Re Construction/Building). Tunapoendelea mbele hatutachoka wala kurudi nyuma kwenye kusimamia yote yanayohusu kujenga Umoja na Mshikamano wa Taifa letu.

***Ndugu Watanzania;***

Mkusanyiko wetu leo hapa, sio kwa ajili ya kuzawadia walioshinda kwenye uchaguzi, la hasha; bali ni matakwa ya kikatiba ya kukabidhiwa dhamana ya kuwa mtumishi mkuu wa Taifa katika kuleta maendeleo endelevu; kwa maana ya uimara wa Kiuchumi, Kisiasa, kidiplomasia na Kijamii. Ili tuweze kuyatimiza hayo, hatuna budi kuhakikisha tunahimizana umoja na upendo kwa nchi yetu, tunadumisha amani na kuheshimu sheria za nchi. Kinyume cha hayo, Maandamano, vurugu na uvunjifu wa amani, husababisha maumivu na havileti manufaa wala faida kwa yeyote. Niwasihi Watanzania tuchague hekima badala ya ghadhabu; busara badala ya mihemuko; upendo badala ya chuki; uvumilivu badala ya vinyongo; umoja badala ya mgawanyiko; amani badala ya vurugu; unyenyekevu badala la kiburi; na huruma badala ya hasira. Taifa letu ni bora na lina nguvu zaidi kuliko mtu yeyote. Demokrasia haipimwi kwa nani kashinda uchaguzi, bali kwa jinsi tunavyoendesha mambo yetu baada ya uchaguzi. Tutakuwa na nguvu zaidi pale kila sauti, chanya na hasi, zinaposikilizwa, kuheshimiwa na kuthaminiwa, na vile vile, tunapoweza kuponya penye maumivu. Hii si kazi ya upande mmoja wa Serikali peke yake, bali ni kwa kila

Jumuiya za Wananchi, Chama cha Siasa, Dini zetu, na kila mwananchi. Na hapa, nitumie fursa hii, kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu Viongozi wa Dini waliohimiza amani na upendo katika kipindi chote cha uchaguzi.

***Ndugu Wananchi;***

Nimeamua kutumia jukwaa hili leo kushukuru na kupongeza kwa kumaliza uchaguzi, kuhimiza Umoja na Mshikamano wa Kitaifa na kusisitiza kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Taifa ni muhimu zaidi kuliko matakwa binafsi ya mtu yeyote. Masuala ya mwelekeo wa kazi za Serikali kwa miaka mitano ijayo, na ufafanuzi wa kina wa hatua zitakazochukuliwa kutekeleza dhana ya Kazi na Utu utatolewa katika hotuba ya uzinduzi wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya kusema hayo, niwashukuru wote kwa kujumuika nasi kwenye tukio hili muhimu na la kihistoria. Nimepokea pongezi zote kwa heshima kubwa, na sasa safari ya kuwatumikia Watanzania kwa kipindi cha pili inaanza rasmi.

***Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.***

***Mungu Ibariki Afrika...!***

***Mungu Ibariki Tanzania...!***

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

# SALAMU ZA PONGEZI

Wakili Mkuu wa Serikali, **Dkt. Ally Possi** kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, anatoa pongezi kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa na kuapishwa kuwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania





## HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, WAKATI WA KUFUNGUA RASMI BUNGE LA 13 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, DODOMA, TAREHE 14 NOVEMBA 2025

### UTANGULIZI

***Mheshimiwa Spika;***

Naanza na wingi wa shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo. Kwa mujibu wa Ibara ya 91, Ibara ndogo ya kwanza, ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana dhima ya kulifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kwa msingi huo, leo nipo hapa kulihutubia Bunge ili kutimiza matakwa ya Ibara hiyo ya Katiba.

Kabla ya kufanya hivyo, nianze na jambo la huzuni lililotokea hapa nchini. Niwaombe tusimame kwa dakika moja kuomboleza na kuwaombea ndugu zetu waliopoteza maisha katika vurugu zilizotokea siku ya Uchaguzi Mkuu tarehe 29/10/2025.

Mimi binafsi nimehuzunishwa sana na tukio lile. Natoa pole kwa familia zote zilizopoteza wapendwa wao, na tunamuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Aidha, kwa majeruhi tunawaombea wapone kwa haraka, na kwa wale waliopoteza mali zao tunawaomba wawe na stahamala na uvumilivu. Serikali imechukua hatua ya kuunda Tume ya kuchunguza yaliyotokea (*Enquiry Commission*) ili tujuwe kiini cha tatizo. Taarifa hio itatuongoza kujielekeza kwenye mazungumzo ya kuleta maelewano na amani.

***Mheshimiwa Spika,***

Baada ya kueleza sononeko hilo, nijielekeze sasa kukupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na kwa kupata imani ya Waheshimiwa Wabunge waliokuchagua kuwa Spika wa Bunge hili la 13. Ni imani yangu kuwa uzoefu wako katika Bunge hili utakuongoza kusimamia utekelezaji wa shughuli za Bunge kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Spika Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuliongoza vyema Bunge la 12. Serikali inaahidi kutoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge hili la 13.

Kwa kauli hiyohiyo, nimpongeze pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili.

Aidha, nirejee pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemb, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameapishwa leo asubuhi.

Niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na Watanzania kuwawakilisha, katika kazi adhimu ya kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali kupitia Bunge hili la 13. Waheshimiwa Wabunge, Hii ni dhamana na dhima kubwa sana mliyopewa na wananchi, na vivo hivyo, matarajio ya wananchi kwenu ni makubwa pia. Matarajio yao ni kuwa mtatumia muda wenu mwingi kuwa na mijadala inayoakisi raha na karaha wanazoziona, na mtaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya kutatua changamoto zao, na kwamba wakati wote mtajielekeza kulinda maslahi ya wananchi waliowachagua, na maslahi mapana ya Taifa.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa vigezo vyovyote vile, Bunge hili ni jipya. Takwimu zinaonesha kuwa Wabunge **223** kati ya Wabunge **393**, sawa na asilimia **56.7** ni Wabunge wapya kabisa. Aidha, asilimia **40.5** ya Wabunge wote ni Wanawake. Wabunge Wanawake waliogombea majimboni safari hii ni **36** ikilinganishwa na Wabunge **21** katika Bunge lililopita. Takwimu hizi zinatueleza kuwa Uchaguzi Mkuu umeleta mabadiliko makubwa kwa kuongezeka kwa idadi ya Wabunge Wanawake walioshinda kupitia majimbo; na kuongeza idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum.

***Mheshimiwa Spika,***

Uchaguzi Mkuu wa kuchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano; Rais wa Zanzibar; Wabunge; Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi; na Madiwani ulifanyika **tarehe 29 Oktoba, 2025** nchini kote. Watanzania kwa mamilioni walijitokeza kupiga kura na kuchagua viongozi waliowataka. Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kujenga mshikamano na umoja wa kitaifa, ili sote kwa pamoja tuijenge, tuitunze na tuilinde nchi yetu, na kuzidi kunyanyua hadhi ya Taifa letu.

Nitumie nafasi hii kuwashukuru tena wananchi wa Tanzania kwa kujitokeza na kushiriki vyema kwenye hatua zote, kuanzia kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura; kuhakiki daftari na kupiga kura. Kwa mara nyengine tena wananchi wamethibitisha kuwa kushiriki uchaguzi ndio njia ya uhakika na ya salama ya kubadilisha viongozi wasioridhika na au wasioridhika na huduma zao. Njia nyingine zozote hazina kheri wala salama ndani yake.

Niendelee kuipongeza Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuendesha vyema Uchaguzi Mkuu wa kwanza tangu kuundwa upya kwa Tume hiyo. Safari hii Wakurugenzi wa Halmashauri hawakusimamia uchaguzi, wala hakuna Mgombea aliyepita bila kupingwa. Sisi tuliogombea na vyama vyetu, hatukukosa viwanja vya kufanyia mikutano. Kwa ujumla, kampeni zilikwenda vyema. Aidha, utaratibu uliofanyika wa kuongeza vituo vya kupigia kura ulisaidia sana kuondoa msongamano katika vituo hivyo. Kwa hakika, upigaji wa kura ulirahisishwa sana na haukuchukua muda mwingi wa wananchi kama ilivyozoeleka. Jambo hili limewafanya baadhi ya waangalizi wa uchaguzi kudhani kwamba wananchi hawakujitokeza kupiga kura.

***Mheshimiwa Spika;***

Pamoja na kuwa uchaguzi ulifanyika, kulijitokeza vurugu na uvunjifu wa amani ambao ulisababisha uharibifu wa mali, kupoteza maisha na kuhatarisha usalama wa Nchi. Tunapoenda mbele, niwasihi sana Watanzania tuongozwe na dhamira ya maelewano, ushirikishwaji, kujirekebisha, na umoja.

Kwa wanangu, vijana wa taifa hili la Tanzania, niseme kuwa Nchi hii imejengwa kwenye misingi ya amani na utulivu wa kisiasa. Sisi wazazi wenu tungeshawishika kuyafanya mliyoyafanya wakati huu, nchi hii isingekuwa na neema na maendeleo mnayoyaona leo. Niwasihi sana wanangu, nchi hii ni yenu, kwa shida zozote zile zinazowakabili, msikubali hata siku moja kushawishiwa kuichoma nchi yenu wenyewe. Msikubali kukata tawi la mti ambalo mmeukalia. Hili nawaomba mlikatae kwa nguvu zenu zote. Ninyi ndio walinzi na wajenzi wa Taifa hili, nawasihi kamwe msije kuwa Wabomoaji wa Taifa lenu.

Kuna wakati vijana hufuata mkumbo wa uhalifu kwa ushabiki, ninatambua kwamba vijana wengi waliokamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhaini hawakujua wanachokifanya. Nikiwa Mama na Mlezi wa Taifa hili, ninavielekeza vyombo vya sheria na hasa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuangalia kiwango cha makosa yaliyofanywa na vijana wetu. Kwa wale ambao wanaonekana walifuata mkumbo na hawakudhamiria kufanya uhalifu wawafutie makosa yao.

Ninatoa msamaha huo kwa sababu, hata maneno ya Mungu katika Kitabu cha LUKA sura ya 23 Mstari wa 34 yanasema, na hapa nanukuu: *“Yesu akasema, Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo.”*

Ndugu zangu Watanzania, tujifunze kutokana na mapito yetu, hapana shaka kwamba Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya kidemokrasia, ila, demokrasia kamili inaweza kutafsiriwa kwenye mitazamo tofauti (haina formula moja). Kama Taifa tunaendelea kujifunza na kujirekebisha. Hivyo basi, sote kwa umoja wetu tunapaswa tuitumie fursa hii tuendelee kujifunza, tujirekebishe na tukubaliane jinsi ya kuiendesha nchi yetu kidemokrasia kwa kuzingatia tamaduni, mila na desturi zetu na sio za kuletewa. Kama tulivyoagizwa na Ilani ya CCM ya mwaka 2025 hadi 2030, moja ya hatua itakayotufikisha kwenye maelewano hayo ni marekebisho ya Katiba yetu. Serikali imeahidi kuanza kulifanyia kazi suala la mabadiliko ya Katiba ndani ya siku mia za muhula wa pili wa Awamu ya Sita kwa kuanza na Tume ya Usuluhishi na Maelewano.

***Mheshimiwa Spika;***

Tunapozungumzia umoja wa Kitaifa tunaongozwa na uwepo wa Tunu ya Muungano wetu. Hivyo basi, kuudumisha kuimarisha na kuuenzi Muungano wetu kutaendelea kuwa kipaumbele cha Serikali tunayoiunda. Tutaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha tunatatua changamoto za Muungano kila zinapojitokeza.

***Mheshimiwa Spika;***

Serikali ya Awamu ya sita iliendeleza tuliyoyaanza katika awamu wa tano, na hivyo kaulimbiu yake ilikuwa **'Kazi Iendelee'**. Ninyi ni mashahidi kuwa kazi iliendelezwa na mengi yalikamilishwa, kama nilivyoeleza katika hotuba ya kufunga Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Juni mwaka huu 2025. Niwahakikishie katika miaka

mitano ijayo tutalinda na kuendeleza mafanikio haya pamoja na kuleta mafanikio mengine na makubwa zaidi.

Katika kipindi cha Kampeni, mimi na Mgombea Mwenza tulitembea nchi yote kuomba kura, na tulisikiliza na kuyabeba matakwa na mahitaji ya wananchi katika kuijenga nchi yetu kwa maisha bora zaidi ya baadae. Tuliwaahidi kuwa, wakitupa tena dhamana ya kuongoza Taifa letu, tutajielekeza katika kutekeleza kauli mbiu ya **'Kazi na Utu, Tunasonga Mbele'**. Yaani, kuhakikisha kuwa jitihada zozote tunazozichukua za kuleta maendeleo, zitalenga kuinua na kuongeza thamani ya utu wa watu wetu wa Tanzania. Hakika tulisikiliza na kuelewa matamanio ya wananchi ya kupata Serikali inayoshughulikia changamoto zao, kama vile; suala la gharama za maisha, kuongeza fursa za kazi na ajira ili waweze kujiendeleza kiuchumi; na kuimarisha ustawi wa jamii zetu. Nataka niwahakikishie kwamba Serikali itachochea upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kujenga matumaini kwa vijana, Wanawake, makundi ya wenye ulemavu, na hata wazee kuanzia mijini mpaka vijijini.

***Mheshimiwa Spika;***

Nianze na masuala ambayo niliwaahidi wananchi kuwa tutaanza nayo ndani ya siku 100 za mwanzo za kazi. Kwanza kabisa linahusu utumishi na utawala bora, nalo ni suala la uundwaji wa Serikali. Niliwaahidi wananchi kuwa Serikali nitakayoiunda itawajibika na kuendelea na mageuzi ya sera zinazogusa maslahi na ustawi wa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Hivyo basi, ni lazima viongozi wa Serikali kwa ngazi zote, kuanzia Mawaziri hadi Maafisa Tarafa, wawe karibu na wananchi ili kuweza kufahamu changamoto zao na kuwajibika kwao. Kwa kuwa ahadi tulizotoa ni nyingi, matamanio ni mengi, matarajio ni makubwa, na muda wa kuyatimiza haya ni mchache, tutaongeza kasi ya utekelezaji wa mipango ya Serikali ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea. Nayasema haya mapema kwa watendaji waliopo Serikalini, wakiwemo Makatibu Wakuu, na wale nitakaowateua kwa ajili ya kujitayarisha kisaikolojia na kujipanga vyema kufanikisha malengo hayo. Wananchi wanahitaji mabadiliko chanya kwa maendeleo. Watendaji msipobadilika, kuendana na matarajio ya wananchi, tutawabadilikia!

***Mheshimiwa Spika;***

Katika hotuba ya kufungua Kampeni tarehe 28/08/2025 nilitaja mambo ambayo Serikali ingeanza nayo ndani ya siku 100 za kazi.

Tuliahidi kutoa ajira kwa fani za Sekta ya Afya na Elimu. Leo ikiwa ni siku ya kumi na mbili tangu muhula huu wa pili wa Awamu ya Sita uanze, tayari tumeshatangaza nafasi za ajira **7,000** za walimu na nafasi za ajira **5,000** za watumishi wa afya. Hatua hii ni ya mwanzo kujibu kiu ya wananchi ya kuboresha huduma za afya na elimu.

Katika hatua nyingine, tunajiandaa kuanza kwa majaribio ya Bima ya Afya kwa Wote. Serikali itakuja kwenu Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo ya namna ya kufanikisha majaribio hayo, na niwaombe muunge mkono mapendekezo hayo ambayo yatakuwa mwanzo wa mageuzi katika upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wote nchini. Tunadhamiria pia kuviunganisha vituo vya huduma za afya kidijitali na kuhakikisha vinakuwa na vifaa na huduma za viwango stahiki kwa kila ngazi husika. Tunakusudia kuweka viwango vinavyofanana ili watumiaji wa bima ya afya mijini na vijijini wawe na huduma zinazolingana.

Katika hatua nyengine, nimeshaielekeza Wizara ya Afya kusimamia maelekezo ya kutozuiwa maiti kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, wakati familia zikiendelea na taratibu za kulipa deni la matibabu kwa njia zinazolinda utu wao. Niseme kwamba, ni kupitia mpango huu wa bima ya afya, kadhia hii inakwenda kukomeshwa. Kwa sababu gharama za matibabu zitalipwa na bima ya anayetibiwa. Niwasihi wananchi wote kuweka kipaumbele kwa afya zetu, kwa kila mmoja wetu kuwa na bima ya afya pamoja na wanaomtegemea.

***Mheshimiwa Spika;***

Ilani ya CCM ya 2025-2030 imeahidi na mimi nilitangaza ahadi hiyo kuwa nitaunda Tume ya kuanzisha Mazungumzo ya Maridhiano na Upatanishi na kuandaa mazingira ya kuanza kwa Mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Hata hivyo, kutokana na uvunjifu wa amani uliotokea nchini, tunahitaji kufanya tathmini ya kina ili tujue kiini na sababu ya kadhia hiyo, na ndipo tuunde Tume ya Maridhiano.

Katika Muhula kwa kwanza wa Awamu ya sita tulikuja na falsafa ya **R4** ili kuliunganisha Taifa. Serikali ilionesha utayari wakati wote kuleta maridhiano, ili kwa pamoja tuweze kulijenga na kulitunza Taifa letu. Serikali ilinyoosha mkono kuwavuta na kuwakaribisha Vyama vya Siasa, Vyama vya Kijamii, Sekta binafsi na hata Jumuiya za Kimataifa, ili kwa pamoja tuijenge Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, mkono huo wa urahimu ulileta matumaini kwa nchi, kabla ya baadhi ya wadau kuamua kuuachilia au **Kuuputa** mkono huo. Kwa kuwa wananchi wa Tanzania wamenipa ridhaa ya kuendelea kuiongoza nchi hii, **sitachoka kunyoosha tena mkono wa maridhiano**. Ni matumaini yangu kuwa wadau wa kisiasa wataupokea kwa dhati mkono wa maelewano, ili kwa pamoja tujenge mazingira muafaka kwa maendeleo ya Taifa letu. Tutajifunza kutokana na makosa na mapungufu ya taasisi zetu za kidemokrasia. Tanzania inauzoefu wa miongo mingi ya demokrasia na amani. Tanzania ina Demokrasia iliyokomaa hata hivyo tutaendelea kuiboresha kulingana na mazingira na wakati. Ni jukumu letu sasa kujielekeza kwenye maboresho hayo kwa utashi wetu bila shinikizo lolote.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa kuwa zaidi ya asilimia 60 ya watu wa Nchi hii ni Vijana, tutaweka kipaumbele kwenye sera na programu zitakazopanua fursa za kiuchumi, kutengeneza kazi na ajira, kuongeza wigo wa hifadhi za jamii, na kuwajengea kesho iliyo bora zaidi.

Ili kuhakikisha vijana wanapata nafasi ya kushiriki katika kujenga mustakabali mwema wa Taifa letu, tutaweka kipaumbele kwenye ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya Maendeleo yao. Natambua kumekuwa na majukwaa mengi ya kuwafikia vijana ila bado shughuli zao zinafifishwa na masuala ya kisiasa, na majukwaa hayo kupoteza malengo na mvuto kwa vijana. Mimi na wenzangu tumefikiria kuwa na Wizara kamili itakayoshughulika na mambo ya vijana, badala ya kuwa na Idara ndani ya Wizara yenye mambo mengi. Vile vile, ninafikiria kuwa Washauri wa masuala ya vijana ndani ya Ofisi yangu.

Jambo jengine tuliloahidi kulitekeleza ndani ya siku 100 za awali za kazi ni kuchukua hatua za kuongeza mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za Vijana na Wanawake kwa kutenga shilingi **bilioni 200**. Serikali inaendelea kuangalia njia nzuri ya kuimarisha mfuko huo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa walengwa. Aidha, kwa

kushirikiana na sekta binafsi, tutaanzisha madirisha ya uwekezaji kwa Vijana (*Youth Investment Windows*). Madirisha haya yatatoa mikopo nafuu na mitaji ya uwekezaji kwa biashara za vijana.

***Mheshimiwa Spika;***

Pamoja na hayo niliyoyaeleza, kuna mengi zaidi ambayo tumejipanga kuyafanya katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Ni dhima ya Serikali kuendeleza ukuaji wa Uchumi. Katika kipindi hiki tutaanza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 hadi 2050, tukilenga kujenga Taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Dira mpya imeweka vigezo vya kuchagua sekta na maeneo ya kupewa kipaumbele yaliyobainishwa kwenye andiko la Dira yenyewe. Kati ya mikakati itakayofanyiwa kazi ni kuwekeza zaidi kwenye sekta zinazoajiri watu wengi na miongoni mwa sekta hizo ni kilimo, utalii, viwanda, ujenzi na madini.

Malengo yetu ya kiuchumi ni kupandisha kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka **asilimia 5.6** ya sasa hadi zaidi ya **asilimia 7** kuelekea mwaka 2030. Ukuaji huu utaiwezesha Serikali kuboresha huduma za kijamii na kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi. Tutaimarisha masoko ya mitaji kwa kuhamasisha uwekezaji wa ndani, na kutumia rasilimali zetu kama madini kudhamini mikopo ya uwekezaji, badala ya kuweka mzigo mkubwa kwenye Deni la Taifa. Mwelekeo wetu ni kukua kwa pamoja kwa uchumi unaogusa maisha ya mtu mmoja mmoja (*Micro economy*) na uchumi jumla (*Macro economy*).

***Mheshimiwa Spika;***

Mtakubaliana nami kuwa Sekta Binafsi ni nguzo muhimu ya ukuzaji wa uchumi, hususan Sekta Binafsi ya ndani. Tutaboresha zaidi mazingira ya biashara nchini kwa kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Aidha, tutatekeleza mapendekezo ya Tume niliyoiunda ya Kuboresha Mifumo ya Kodi nchini ili kuwapatia wafanyabiashara wetu wepesi katika kufanya biashara zao.

Tutaendelea kuweka nguvu zaidi kudhibiti mfumuko wa bei za bidhaa ambayo ni hatua muhimu katika kupunguza gharama za maisha kwa Wananchi. Pia tutaweka motisha kwa viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuuza kwenye soko la ndani na nje. Tutaongeza vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi ili kuchochea uzalishaji na kukuza ushindani wa bidhaa za ndani.

Mbali na mikopo, tutafungua fursa mahsusi kuhamasisha vijana na wamiliki wa biashara ndogo kupata elimu ya biashara na kuweza kujisajili katika Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Serikali (TANSIS).

Vile vile, kupitia vyuo vyetu vya ufundi stadi VETA tutaongeza programu maalum za mafunzo ya ufundi stadi na kuunganisha programu hizi na miradi ya mikakati kama reli ya kisasa (SGR), uendelezaji wa bandari, uchumi wa buluu, madini na gesi ili vijana hawa wapate uzoefu na waweze kuajirika. Serikali itaanzisha Kanda za Kuendeleza Ujuzi zitakazowawezesha vijana kupata ujuzi unaohitajika katika makampuni ya sekta binafsi, na kuangalia uwezekano wa kutoa vivutio maalum kwa makampuni yatakayotoa nafasi nyingi za ajira kwa vijana. Aidha, tutaweka mazingira ya kuhakikisha tunakuza vijana kwenye uongozi kwa kuwezesha vyuo vyetu kufanya mafunzo ya ulezi na ukuzaji wa vijana viongozi (mentorship).

Tutataizama mikopo ya **asilimia 10** ya makusanyo ya Halmashauri zetu ili kuboresha upatikanaji wa mikopo hiyo kwa walengwa. Vile vile, ni vyema walengwa wakajua kwamba Fedha hizi ni mkopo na sio msaada, ni mbegu na sio mavuno na ni mtaji na sio ruzuku, hivyo marejesho na tija yake lazima ionekane. Matamanio yangu ni kuona ifikapo mwaka 2030, tuwe tumetengeneza wawekezaji vijana ambao watatoa ajira kwa vijana wenzao.

Kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo tutahamasisha ufadhili kwa biashara za wanawake, Ili kuwasaidia wanawake wanaofanya kazi kwenye masoko, tutaongeza na kuratibu kwa karibu Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kurasimisha biashara zao na kuwawezesha kukopesheka. Tutawekeza katika kuboresha miundombinu ya masoko, mifumo ya maji safi na maji taka, huduma za afya, na vituo vya matunzo ya watoto kwenye masoko.

Katika hatua nyingine, tutalipa kipaumbele suala la kutenga maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili Serikali iwatambue na kuwarasimisha ili waweze kufanya kazi zao bila bughudha na wachangie kwenye Pato la Taifa. Kwa rasilimali ambazo nchi yetu imebarikiwa na nguvu kazi kubwa tuliyonayo, ninaamini tunaweza kabisa kujipanga na kufikia lengo hilo. Kwa kufanya hivyo, ndio tutafikia lengo letu la kuzalisha ajira milioni 8.5 katika sekta mbalimbali ifikapo mwaka 2030.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande wa huduma za kijamii, maendeleo makubwa yamepatikana kwenye sekta ya maji, ambapo hali ya upatikanaji wa maji ilipanda kutoka **asilimia 84** hadi **asilimia 91.6** mijini, na kutoka **asilimia 70.1** hadi **asilimia 85** vijijini. Tumefika pazuri kuliko pale tulipokuwa mwaka 2021. Hata hivyo, azma ya Serikali ni kufikia asilimia 100 ya upatikanaji wa maji safi, salama na uhakika. Hivyo tunakwenda kuongeza nguvu ili kuyafikia yale maeneo machache ambayo upatikanaji wa maji bado ni changamoto.

Katika miaka 5 ijayo, tutakamilisha ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji ambayo itategemea maji kutoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Tutakamilisha miradi mikubwa ya maji inayoendelea ikiwemo miradi ya maji ya miji 28, na miradi mikubwa ya bwawa la Kiwira (itakayohudumia Mbeya), bwawa la Kidunda, Bonde la Mto Rufiji (itakayohudumia Dar es Salaam, Lindi na Pwani), Same-Mwanga-Korogwe (itakayohudumia Kilimanjaro na Tanga), na upanuzi wa Capri Point (itakayohudumia Mwanza), kwa kuitaja kwa uchache.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwenye sekta ya afya, mbali na masuala ya Bima ya Afya kwa Wote, na ongezeko la ajira za watumishi wa afya ambayo nimeshayagusia, tutakamilisha ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati zinazojengwa kote Nchini. Tutaendelea kuboresha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuongeza uwezo wake kutoka vitanda **1,435** vya sasa hadi vitanda **1,757** ifikapo 2030. Itakapokamilika, itaweza kutoa huduma za kibingwa na kuwa hospitali ya kutumainiwa na kukimbiliwa katika Afrika ya Mashariki.

Tutaongeza huduma za kibingwa za afya kwenye hospitali zetu za rufaa za Mikoa na hospitali za rufaa za Kanda, ili tuwapunguzie gharama wananchi kutafuta huduma za rufaa nje ya Mikoa yao. Tunataka, badala ya kuwa na watu kuzifuata huduma, huduma ziwafuate watu.

Tutaendelea kuwekeza katika kujenga uwezo wetu wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko. Tumejipanga kujenga hospitali kubwa ya Kitaifa ya magonjwa ya mlipuko na tutaijenga Mkoani Kagera.

Vilevile, tutajielekeza katika kuongeza uwezo wa uzalishaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kupunguza uagizaji na kupunguza gharama za matibabu. Katika hili, tutavihakikishia viwanda vya ndani soko la uhakika kupitia Bohari ya Dawa (MSD).

Halikadhalika, tutakuza utafiti, utambuzi na utoaji wa ithibati wa dawa zetu za asili. Baada ya uwekezaji huu tutajielekeza zaidi kwenye kinga (*preventive medicine*) tofauti na sasa ambapo tumejikita zaidi kwenye tiba (*curative medicine*) pekee.

Aidha Serikali inatambua mchango wa Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za afya na ahadi yetu ni kuendeleza ushirikiano huu.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande wa Elimu, katika miaka mitano ijayo tunaanza utekelezaji kamili wa maboresho ya Sera ya Elimu inayosisitiza elimu ujuzi. Tutaendelea kuweka mkazo zaidi kwenye masomo ya sayansi na hisabati (STEM). Azma yetu ni kuongeza wanasayansi wabobezi katika eneo la sayansi ya data, akili unde, sayansi ya kompyuta na teknolojia za viwanda. Tutatumia Mfuko wa *Samia Scholarship* kusomesha wanasayansi hawa ndani na nje ya nchi. Jambo hili litakwenda sambamba na kukamilisha shule maalum za Sekondari za Wasichana za Sayansi na zile za vipaji za Wavulana katika kila mkoa. Ili kuhakikisha mitaala na silabasi zetu zinatekelezwa kikamilifu, tutaunganisha kwa njia ya kidijiti shule za vijijini na mijini ili kubadilishana uzoefu na taarifa.

Kama tulivyowaahidi wananchi, tutaongeza mikopo ya elimu ya juu, kwani kipindi hiki kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tutakuwa na kampasi za vyuo vikuu

kila mkoa. Vilevile, tutasimamia mpango wetu wa kuhakikisha kila Wilaya ina chuo cha VETA chenye vifaa stahiki vya mafunzo kwa vitendo.

***Mheshimiwa Spika;***

Nilishagusia suala la kuongeza walimu. Pamoja na walimu, tunaenda kuwekeza zaidi pia kwenye miundombinu ya shule za awali, msingi na sekondari mpya pamoja na kuongeza madarasa kwenye shule zilizopo.

Tunapotekeleza maendeleo jumuishi, tutaendeleza jitihada tulizizianza za kuweka miundombinu na vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; pamoja na hao, tutaendeleza fursa muhimu ya kuwasomesha na kujiendeleza kwa watoto wenye magojwa adimu (*rare diseases*) wanaohudumiwa majumbani.

***Mheshimiwa Spika;***

Katika miaka mitano ijayo, tunaenda kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta za uzalishaji, tukianza na kilimo. Tutaongozwa na dhana ya "**Kilimo ni Biashara, Mkulima ni Mwekezaji**". Lengo letu ni kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hii kutoka asilimia **4** ya sasa hadi kufikia asilimia **10** ifikapo mwaka 2030. Kwa kufanya hivyo, tunalenga sio tu kujihakikishia utoshelevu wa chakula, bali pia tutawekeza kwenye mnyororo wa thamani ili kuwanufaisha Watanzania wengi walioajiriwa kwenye sekta hii. Tunakusudia kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya mahindi, mchele na mbogamboga (*Horticulture*), barani Africa.

Tutafanya hivyo kwa kujielekeza kwenye kilimo cha kisasa kwa kuongeza pembejeo kama mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa ruzuku, tutaongeza **upatikanaji wa maji ya uhakika** na kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka **ekari milioni 3.4** hadi ekari milioni **5**, kwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa na skimu za umwagiliaji zinazoendelea na kuanzisha skimu mpya ikiwemo kwenye bonde la Mto Rufiji. Aidha, tutaanzisha vituo vya ukodishaji zana za kilimo, ambavyo vitatoa huduma za **matumizi ya teknolojia katika kilimo chetu**. Ili kukuza uwekezaji kwenye sekta ya Kilimo, tutaziimarisha benki zetu za Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Ushirika ili zichochee mapinduzi tunayoyatazamia.

***Mheshimiwa Spika;***

Pamoja na kuongeza uzalishaji, lazima pia tudhibiti upotevu wa mazao baada ya mavuno (*post harvest loss*). Hivyo, tutaendelea kuwekeza katika kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao chini ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Aidha, tutazidi kuboresha mifumo ya stakabadhi ghalani ambayo imeshaanza kuwaletea manufaa wakulima wa mazao mbalimbali yaliyojumuishwa kwenye mfumo huo. Katika kupanua masoko yetu nje, na kutumia fursa za diplomasia yetu ya uchumi kuyatumia masoko ambayo tayari tulishafungua, tutahakikisha kuwa fursa hizi zinakuwa na makubaliano yanayotekelezeka ili kuwa na uhakika wa masoko haya. Hapa tunakusudia masoko ya mbaazi, choroko na ufuta, kupata masoko ya uhakika.

Pamoja na kujitosheleza kwa chakula kwa **128%** kwa sasa, mwelekeo wetu ni kuendelea kupiga hatua kwenye uzalishaji wa sukari na mafuta ya kupikia hususan uzalishaji na usindikaji wa alizeti, chikichi na ufuta.

***Mheshimiwa Spika;***

Kuna mazao ya biashara ambayo yalikuwa yakifanya vizuri sana na kuwanufaisha wakulima wengi, lakini yameathiriwa na ama bei za soko duniani, au wawekezaji waliopewa viwanda vya kuchakata mazao hayo kushindwa kuviendesha vyema viwanda hivyo. Tutayasimamia kwa karibu zaidi mazao ya Chai, Kahawa, Parachichi na Pamba tukiwa na shabaha ya kupanua masoko, kuongeza ushindani wa bei na kuwafaidisha zaidi wakulima wetu.

***Mheshimiwa Spika;***

Serikali imeanza kuona fursa na kuleta mageuzi kwa sekta ya Ufugaji. Miongoni mwa ahadi zetu kubwa ni kuongeza eneo lililopimwa na kutengwa kwa shughuli za ufugaji kutoka ekari milioni **3.46** hadi ekari milioni **6.** Hatua hii itaepusha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, na itaongeza wigo wa uzalishaji wa malisho ya mifugo ili tuelekee kwenye ufugaji wa kisasa. Katika hatua za kuyafungua masoko ya kimataifa, tutaendeleza Chanjo, pamoja na Utambuzi wa mifugo yetu nchini, ili kuongeza ubora wa mazao ya mifugo, tuweze kuingia kwenye kumbukumbu za Dunia na kutambulika sokoni.

Pamoja na hatua hiyo, tutaendelea na kuboresha kosafu (sifa) za mifugo, kujenga Mabwawa ya kunyweshea, majosho, machinjio na miundombinu mingine muhimu kwa ajili ya ufugaji. Lengo ni kuwa na mnyororo wa kuongeza thamani ya mifugo na mazao ya mifugo, kwa ajili ya kuliendea soko la nje. Tutoke kwenye kumtazama ng'ombe na mlio wake, tutazame uzito wa nyama, ladha ya nyama, wingi wa maziwa, ubora wa ngozi, ubora wa kwato na pembe. Mtazamo huo ndio utakaoleta mapinduzi ya sekta ya mifugo.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwenye uvuvi, tunaenda kuongeza manufaa ya uvuvi wa Bahari Kuu na kwenye Maziwa Makuu. Tutakamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi iliyopo Kilwa, ambayo itazalisha fursa za ajira takriban elfu thelathini (30,000). Tutajenga bandari nyingine ya kisasa ya uvuvi kule Bagamoyo itakayofungamanishwa na kongani ya viwanda vya samaki. Tutafanya mapitio ya utoaji wa leseni za uvuvi kwa lengo la kuifanya nchi kufaidika ipasavyo na fursa za uvuvi wa bahari kuu.

Aidha, tutaendeleza utoaji wa mikopo ya boti, zana za uvuvi, makasha ya kuhifadhi samaki na miundombinu ya kukaushia. Vilevile, tutawekeza zaidi kwenye vizimba na mabwawa ya kufugia samaki, na kuwawezesha wananchi wengi zaidi kuongeza kipato na kujikwamua kiuchumi. Hili litakwenda sambamba na kutafuta majawabu ya teknolojia ya chakula cha samaki ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kwa wafugaji wa samaki (*aquaculture*).

Tutalipa kipaumbele suala la maendeleo ya uchumi wa buluu na sekta ya uvuvi, ikiwemo kilimo cha kisasa cha mazao ya baharini.

***Mheshimiwa Spika;***

Hatuwezi kufikia malengo yetu bila kuikuza sekta ya viwanda nchini. Hivyo, tumejiwekea lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani kutoka asilimia **4.8** hadi kufikia asilimia **9** kwa mwaka ifikapo **2030**.

Katika kipindi kilichopita tuliweza kuanzisha kongani kubwa za viwanda na kuvutia wawekezaji wengi zaidi, ikiwemo kongani ya viwanda ya Kwala ambayo itakapokamilika itazalisha ajira za moja kwa moja laki moja **(100,000)** na zisizo za moja kwa moja laki

tano **(500,000),** na pia Kongani ya Viwanda ya Buzwagi inayotarajia kuzalisha ajira laki tatu **(300,000)** itakapokamilika. Tutaongeza kongani nyingine mpya na ya kisasa kule Bagamoyo ambayo nayo inatarajiwa kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wa Tanzania.

Tunapoanza safari ya muhula wa pili wa miaka mitano ya awamu ya sita, tunajipanga kuweka kongani za viwanda katika kila Wilaya ili tuongeze thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na madini tunayozalisha, na vitakavyoweza kuzalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya maeneo yetu.

Tutahamasisha ujenzi wa viwanda vitakavyolisha viwanda vyengine, kwa malighafi na vipuri, na viwanda vitakavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya kikanda. Lengo la mkakati huu ni kuelekea kwenye Taifa linalojitegemea.

***Mheshimiwa Spika;***

Kuna viwanda ambavyo vimebinafsishwa lakini vimetelekezwa na havifanyi kazi. Hali hii, inakinzana na dhamira njema ya kuvibinafsisha, na pia inawakosesha wananchi soko na fursa za ajira. Kwa kuwa viwanda hivi vilikusudiwa kuongeza thamani ya mazao katika maeneo viliko, tutashirikisha vyama vya ushirika katika kuvifufua na kuviendesha. Lengo la Serikali ni kuona kuwa ushirika una uwezo wa kusambaza pembejeo, kuzalisha zaidi, kuendesha viwanda vya uongezaji thamani ya mazao, na kutafuta masoko pia.

Ili kuitekeleza vyema ajenda yetu ya uchumi wa viwanda, tutaendelea kuimarisha miundombinu wezeshi ya umeme, maji, bandari, reli na barabara kwa ajili ya usafiri na usafirishaji wa malighafi na bidhaa. Tutafanya mapitio ya Sera na Sheria zetu za biashara ili kujenga mazingira wezeshi na bora ya kuvutia biashara na uwekezaji. Vilevile, tutaungana na majukwaa ya kimataifa ya uwekezaji barani Afrika na duniani kuiweka Tanzania katika nafasi ya kuvutia wawekezaji wakubwa Duniani ili kufungua rasilimali zetu.

***Mheshimiwa Spika;***

Tanzania imebarikiwa sana na madini ya aina mbalimbali. Hadi sasa, eneo lililopimwa na kufanyiwa utafiti wa kina ni asilimia **16** tu ya eneo lote lenye miamba yenye madini nchini. Kazi yetu miaka inayokuja ni kuhakikisha madini haya yanawaletea maendeleo wananchi na kuwainua kiuchumi. Katika kipindi kilichopita, tuliweza kuongeza

mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia **6.8** mwaka **2020** hadi kufikia asilimia **10.1** mwaka **2024**. Hatua hii inamaanisha madini yanachangia zaidi mapato kwa wananchi, makusanyo kwa Serikali, na uwekezaji kwenye huduma za kijamii.

Kuelekea mwaka 2030, tutakamilisha Mkakati wa madini adimu (critical minerals) ili Serikali itambue aina ya madini, viwango vya madini na eneo madini yalipo. Kwa kuwa Madini ya Kimkakati ndio yanayohitajika zaidi Duniani, tutaongeza umakini katika kusimamia uwekezaji wa madini hayo.

Katika jitihada zetu za kuendeleza sekta hii ya madini, tutapitia upya leseni zilizotolewa ili kubaini leseni ambazo hazijaendelezwa na kuchukua hatua za kuzitoa kwa wachimbaji wenye nia ya dhati ya kufanya uendelezaji wa maeneo husika. Wachimbaji wadogo wamekuwa nguzo ya kutegemewa katika sekta ya madini nchini. Hivyo basi, tutatenga maeneo maalum kwa ajili yao, tutawapatia leseni na tutawaendeleza kwa kuwapa mitaji na mitambo ya uchorongaji, pamoja na kuwapatia taarifa sahihi za kijiolojia.

Aidha, tutaendeleza utaratibu wa Benki Kuu kununua akiba ya dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na wa kati walio na leseni halali kutoka Tume ya Madini. Tunafanya hivi kuhakikisha wachimbaji wanapata mnunuzi wa uhakika, kupunguza utoroshaji wa madini na pia kurasimisha biashara ya uchimbaji kwa vijana wa Tanzania.

***Mheshimiwa Spika;***

Tutaendelea kuimarisha masoko ya madini na vito. Kipekee kwa madini ya Tanzanite, tunaenda kumalizia jengo la *Tanzanite Exchange Centre* (TEC) katika eneo la Mirerani. Mbali na kuwa Nchi yetu ni mzalishaji mkubwa wa madini, tunataka ifikapo 2030 Tanzania iwe kituo kikuu cha uuzaji wa madini yote katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hatua nyingine muhimu katika kuongeza mchango wa Sekta ya madini katika maendeleo ya nchi ni kusimamia uongezaji wa thamani ya madini hayo hapahapa nchini.

Tunadhamiria kuwa na kiwanda cha kuchenjua madini (*multipurpose refinery*) ifikapo 2030. Tutaondokana na kusafirisha makinikia kwenda nje ili tuokoe ajira ambazo tumekuwa tukizipoteza. Vilevile, tutaanzisha Mfuko wa Wakfu wa Madini (*Minerals*

*Sovereign Wealth Fund*) ili fedha zitokanazo na madini zije ziwafae vizazi vijavyo. Tunafanya hivyo tukitambua kuwa madini si mahindi kwamba ukiyavuna, utatenga mbegu ili uyaoteshe tena. Ukichimba madini kuna mwisho wake. Tunataka vizazi vyetu visikute mashimo tu, bali wakute fedha zitokanazo na madini tunayoyavuna leo.

***Mheshimiwa Spika;***

Tanzania imejaaliwa vivutio vingi vya utalii ambapo sekta hii ina mchango mkubwa sana kwenye uchumi.

Tunapoelekea 2030, tutaendelea kuikuza zaidi sekta hii tukilenga kufikia watalii wa ndani na nje milioni 8. Tunaamini kwamba, kutokana na wingi na ubora wa vivutio pamoja na utajiri mkubwa wa kitamaduni, tunaweza kufikia lengo hili. Sasa ili kukuza utalii tutafungamanisha vivutio vya utalii ili mtalii atumie siku nyingi zaidi akiwa hapa nchini. Vilevile, tutaboresha vyuo vyetu vya utalii na ukarimu, kwa kuongeza idadi ya watoa huduma wenye weledi katika fani zote kwenye hii sekta ya utalii na ukarimu. Sekta hii nayo ni sehemu muhimu ya mpango wa kuzalisha ajira zaidi kwa wananchi na kutuongezea akiba ya fedha za kigeni.

Tutaendeleza pia jitihada za uhifadhi na utunzaji wa maliasili sambamba na kupambana na ujangili. Aidha, hatuna budi kuongeza nguvu kukabiliana na changamoto ya wanyama waharibifu inayokabili jamii mbalimbali zinazopakana na hifadhi kote nchini. Niwaahidi kuwa Serikali itaongeza askari, vituo vya ulinzi, mbinu na vifaa vya kisasa ikiwemo ndege nyuki kukabiliana na athari hizi za wanyama waharibifu.

***Mheshimiwa Spika;***

Eneo lingine tutakalolipa uzito mkubwa ni sekta ya ujenzi. Kipaumbele chetu kitakuwa kukamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ambazo tayari zimeanza na zinaendelea. Tutaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya barabara kupitia TANROADS, ili tufikie lengo letu la kuunganisha Wilaya zote na Makao Makuu ya Mikoa kwa kiwango cha lami.

Kwa jiji la Dar es Salaam, tutaboresha barabara kuu kwa kujenga barabara za juu katika makutano ya barabara katika maeneo ya Morocco, Mwenge, Magomeni na Tabata,

na ujenzi wa awamu zilizobaki za miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT). Tutaijengea uwezo UDART ili iweze kusimamia vyema uendeshaji wa mabasi haya. Tutakamilisha pia ujenzi wa daraja muhimu, Daraja la Mto Msimbazi.

Tutaongeza pia bajeti na uwezo wa TARURA kuboresha barabara za ndani na za vijijini ili kuhakikisha zinapitika mwaka mzima, na kuwa wakulima wanaweza kuyafikia masoko kwa urahisi.

Kwa upande wa ujenzi wa makazi, jitihada zetu zitajielekeza kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi ili tuwawezeshe wananchi kujenga makazi bora. Tutaweka mkazo maalum kwenye nyumba bora na nafuu. Tutasimamia utekelezaji wa sera zinazolenga kuboresha hali ya makazi kwenye maeneo yenye makazi duni. Tutashirikiana na sekta binafsi ili kuongeza uwekezaji kwenye miradi ya uendelezaji miji kwa kujielekeza kwenye ujenzi wa nyumba za bei nafuu (yaani *affordable housing*).

Sambamba na hilo, tutaongeza kasi ya urasimishaji wa maeneo ya makazi, na kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi, kwa kupima ardhi nchi nzima kwa teknolojia ya kisasa ya satelaiti (*Land Geo Spatial Technology*).

***Mheshimiwa Spika;***

Hakuna maendeleo ya kiuchumi na kijamii bila nishati ya umeme wa uhakika na wenye nafuu. Hakuna. Katika kipindi kilichopita tuliweza kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme kutoka **Megawati 1,600** na kufikia **Megawati 4,000** na pia tulifikisha miundombinu ya umeme kwenye kila kijiji. Tunapoelekea mwaka 2030, tumejiwekea lengo la kuongeza uzalishaji wa umeme maradufu kufikia **Megawati 8,000** na tutaendelea kupanua mtandao wa umeme ili kuvifikia vitongoji vyote nchini.

Tutaongeza uzalishaji kwa kutumia vyanzo vya nishati mbalimbali ambazo nchi yetu imebarikiwa nazo ikiwemo maji, jua, gesi, joto ardhi na upepo, na hata umeme utokanao na nguvu ya nyuklia. Vilevile, kupitia mpango wa Gridi Imara tutakamilisha ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji umeme na tutaongeza vituo vya kupoza umeme ili kuhakikisha shughuli za kiuchumi na makazi yanapata umeme wenye nguvu inayotakiwa.

Lengo letu ifikapo 2030, mikoa yote ya Tanzania iwe imeunganishwa na gridi ya Taifa ya umeme.

Ili kuihakikishia nchi usalama wa nishati ya mafuta, tutaboresha miundombinu ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari zetu na maeneo ya kimkakati.

Tutasimamia utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia. Lengo ni kufikia asilimia **80** ya Watanzania wanaotumia Nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034, hatua itakayopunguza uharibifu wa mazingira na kulinda afya za watumiaji.

Kwa upande wa gesi asilia, niwatoe hofu kuwa tupo kwenye hatua nzuri za majadiliano. Tuna dhamira ya dhati ni kukamilisha majadiliano hayo ya mradi huu mkubwa na wa kihistoria wa **dola bilioni 42** wa uchimbaji wa gesi asilia. Kama tutakubaliana na wawekezaji, Mradi huo utabadilisha kabisa taswira na sura ya uchumi wetu. Katika majadiliano yetu tumechelewa kidogo kwa sababu tunahakikisha majadiliano hayo yanazingatia maslahi mapana ya nchi na kuhakikisha mradi huu utawanufaisha Watanzania moja kwa moja. Vilevile, tutajielekeza pia kwenye kuongeza utafiti wa gesi asilia maeneo ya baharini na nchi kavu.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa kuwa Tanzania ni lango kuu la kuzifikia nchi nyingine za Afrika ya Mashariki na kusini mwa Afrika, tunalazimika kuwekeza sana kwenye miundombinu ya usafiri na usafirishaji, ili tuweze kuwahudumia vyema ndugu zetu ambao hawakupata bahati ya kuwa na milango ya kuingia na kutoka kwa njia ya bahari.  Hii ndiyo njia pekee ya kunufaika na fursa yetu ya kijiografia. Ni kwa msingi huo, tunaendeleza uwekezaji kwenye ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR ya ushoroba wa kati kwa kukamilisha vipande vilivyosalia, yaani Makutupora-Tabora; Tabora-Isaka; Isaka-Mwanza; na Tabora-Kigoma, na vilevile, kipande kinachoenda Burundi cha Uvinza-Musongati. Tutakuja na mkakati wa kuhakikisha reli inatengeneza ushoroba wa uchumi, biashara na uwekezaji.

Tunajipanga pia kujenga reli ya SGR kutoka Tanga hadi Musoma, na kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay (Ruvuma) inayofika pia Mchuchuma na Liganga. Sambamba na ujenzi wa reli mpya, tutasimamia maboresho ya reli zilizopo ikiwemo reli ya TAZARA.

Ninafurahi kuwaatarifu kuwa hivi karibuni kutafanyika hafla ya kuweka jiwe la msingi la Mradi wa Ukarabati wa Reli ya TAZARA itakayofanyika nchini Zambia. Aidha, kwa reli ya zamani ya Meter Gauge (MGR) tutafanya ukarabati wa vipande vya Tabora - Kigoma; Kaliua - Mpanda; Tanga - Arusha; Ruvu - Mruazi; ili nayo itumike kuchochea uchumi. Miradi yote hii itazalisha fursa nyingi za ajira kwa Watanzania.

Katika kushirikisha sekta binafsi, tutasimamia ujio wa waendeshaji binafsi kwenye reli zinazojengwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Kwa kuanzia tutakuwa na mwendeshaji binafsi kwenye reli ya TAZARA, hatua hii itazidi kupunguza gharama za usafirishaji kwa wafanyabiashara.

Vilevile, tunakusudia kujenga treni za mijini za kisasa katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kuboresha usafiri kwenye majiji haya yanayokua kwa kasi kubwa sana. Kwa mfano, Dar es Salaam inatarajiwa kuwa na wakaazi milioni **10** ifikapo mwaka 2030, hivyo, kurahisisha njia za usafiri ni kurahisisha shughuli za kiuchumi.

***Mheshimiwa Spika;***

Tukiangazia upande wa uchukuzi, mwelekeo wetu wa kisera ni kujenga Mfumo Fungamanishi, yaani *Multimodal Transport System*, ambao utahakikisha kuwa bandari, viwanja vyote vya ndege, na vituo vya reli vina muunganiko wa usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia mbalimbali.

***Mheshimiwa Spika;***

Baada ya maboresho ya miundo mbinu na mifumo ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, gharama za uendeshaji wa bandari zimepungua ambapo zaidi ya Shilingi **bilioni 258** kwa mwaka zimeokolewa. Fedha hizo zinatumika kuongeza uwekezaji kwenye bandari hiyo ya Dar es Salaam.

***Mheshimiwa Spika;***

Kuelekea mwaka 2030, tutasimamia maboresho zaidi kwenye bandari zetu nchini. Tutaongeza gati 10 kwenye Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa sasa ina Gati **12.** Tutakamilisha kuunganisha reli ya SGR na bandari ili mizigo isafirishwe kwa reli hadi

Bandari Kavu ya Kwala ambapo magari ya mizigo (malori) yatafanya kazi ya usafirishaji kuanzia hapo.

Vilevile, tutazidi kuboresha bandari zetu za bahari ya Hindi ikiwemo Tanga, ambayo tutaiunganisha kwa reli na Bandari ya Musoma kule Mara. Tutafanya upanuzi na maboresho kwenye bandari ya Mtwara ambayo nayo, tunakusudia kuiunganisha kwa reli na Bandari inayojengwa Mbambabay kule Nyasa, Ruvuma. Bandari mpya itakayojengwa Bagamoyo itaunganishwa na Bandari kavu ya Kwala.

Halikadhalika, tutaziendeleza bandari zetu za maziwa makuu za Mwanza, Kigoma, na Kalema kule Tanganyika na tutakamilisha ukarabati na ujenzi wa meli za abiria na mizigo zitakazotoa huduma kupitia bandari hizo, ikiwemo MV Mwanza ambayo imeshaanza kutoa huduma za usafirishaji kule Kanda ya Ziwa. Sambamba na hilo, tutakamilisha upatikanaji wa meli kubwa itakayotoa huduma katika Bahari ya Hindi.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande wa usafiri wa anga, pamoja na mambo mengine, tumepanga kuwa ifikapo mwaka **2030** tuliimarishe zaidi Shirika letu la Ndege la Tanzania kwa kuongeza ndege mpya **8** kuliwezesha shirika kuongeza miruko ndani na nje ya nchi. Mwelekeo wetu ni kufungua nchi pamoja na kukifanya kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kuwa kiungo (*hub*) cha safari za ndege kimataifa.

Aidha, tutakamilisha ujenzi wa viwanja mbalimbali unaoendelea, vikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Msalato - Dodoma, na viwanja vya Mwanza, Iringa na Mpanda. Aidha, tutaongeza viwanja vikubwa hasa vilivyopo pembezoni mwa nchi kwa lengo la kuendelea kupanua biashara na utalii. Miongoni mwa miradi hiyo ni viwanja vya ndege vya Mugumu kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti; Kiwanja cha Ndege cha Njombe kukuza biashara ya mazao na matunda na kurahisisha usafirishaji wake; na Kiwanja cha Ndege cha Kyabajwa, Kagera kitakachofungua fursa zaidi kwa mkoa wa Kagera.

Serikali itajenga Chuo Kikuu cha Anga cha Taifa na kuimarisha mafunzo na kuvutia zaidi wataalam wakiwemo marubani, wahandisi na wahudumu wa ndege.

***Mheshimiwa Spika;***

Tunapotekeleza Mkakati wa Uchumi wa kidijitali, uwekezaji kwenye TEHAMA ni muhimu sana. Hivyo, tutaendeleza kazi ya kuhakikisha mifumo yetu inasomana ikiwemo mifumo mipya inayoanzishwa. Tutaongeza matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo akili unde (*artificial Intelligence*) ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma.

Kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na kampuni za watoa huduma, tutahakikisha huduma ya mtandao inawafikia Watanzania wengi zaidi ili iwasaidie kujiunga katika mifumo ya upatikanaji wa fedha na mitaji (*Financial Inclusion*) na kukuza biashara zao. Tutajenga pia Chuo cha Teknolojia ya Kidijitali (*Digital Technology Institute*) ili kuwajengea vijana wetu uwezo wa kushindana katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia.

***Mheshimiwa Spika;***

Utunzaji wa Mazingira ni suala muhimu sana katika maendeleo tunayoyapanga na kuyatarajia. Kuelekea 2030, tutaimarisha usimamizi wa biashara ya hewa ukaa (*Carbon Trade*) kwa manufaa ya wananchi wa maeneo husika na taifa kwa ujumla. Vile vile hatua hii itasaidia kupunguza migogoro ya mikataba katika siku za usoni.

***Mheshimiwa Spika;***

Tutaendelea kulinda uhuru wa vyombo vya habari ili Watanzania wapate haki yao ya kupata taarifa za ndani na nje ya nchi. Tutaendelea kutoa leseni kwa vyombo vya habari, na kulinda uhuru wa kufanya kazi zao, kwa kufuata sheria za nchi. Tutaimarisha vitengo vya habari vya Serikali ili viweze kutoa habari kwa weledi na kwa wakati. Aidha, tutaendelea kutambua waandishi wa habari za maendeleo nchini kupitia Tuzo ya Samia Kalamu Awards.

***Mheshimiwa Spika;***

Maendeleo ya nchi yoyote yanaonekana katika utamaduni na ustaarabu wake. Isitoshe katika dunia ya leo, utamaduni ni bidhaa na utamaduni ni uchumi. Hivyo, tutakuza na kuifanya lugha yetu ya Kiswahili kuwa bidhaa.

Vilevile, tunaendelea na maandalizi ya ujenzi wa studio ya kisasa ya filamu ili kupandisha thamani ya kazi za wacheza filamu wetu hapa nchini.

Tutajenga ukumbi wa kisasa wa maonyesho ili kuwawezesha wasanii wetu kufanya matamasha ya kimataifa, na kuvutia wasanii wa nje wakubwa kufanya matamasha nchini.

Tunataka sanaa, filamu na muziki zitengeneze ajira na kuchangia uchumi wa Taifa.

***Mheshimiwa Spika;***

Michezo ni uchumi. Hatuwezi kupata matokeo makubwa bila kuwekeza. Miongoni mwa hatua tutakazozichukua ni kuanzisha na kuendeleza shule za michezo (*sports academies*) kwa lengo la kuwaandaa wanamichezo wa leo na kesho.

Kama mnavyofahamu, nchi yetu itakuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON mwaka 2027, na kuelekea huko tutakamilisha ujenzi wa viwanja vitakavyotumika, ikiwemo Uwanja wa AFCON uliopo Arusha, na maboresho ya viwanja vingine nchini. Vilevile, tutaendelea kuvutia michezo mbalimbali kufanyika hapa nchini ili kuongeza fursa zitokanazo na kuwa mwenyeji wa michezo hiyo.

***Mheshimiwa Spika;***

Tanzania inathamini ushirikiano wa kimataifa na ingependa kuishi na mataifa mengine kwa misingi ya kuheshimiana na kufaana. Serikali ina dhamira ya dhati ya kuendeleza mahusiano mazuri yaliyopo na nchi marafiki na mashirika ya kimataifa. Daima tutajielekeza katika kuongeza marafiki, na kupanua fursa za kiuchumi kwa nchi yetu na watu wake.

Kama Taifa, tunapenda tuheshimiwe kama sisi tunavyoheshimu mataifa mengine. Na katika kulinda maslahi ya Nchi, hakuna mbadala. Ni lazima tuhakikishe tunalinda utu, heshima na uhuru wetu. Tutaendelea kuongozwa na misingi ile ile ya Sera ya Nje iliyoasisiwa na waasisi wa nchi yetu ya kutofungamana na upande wowote.

Msimamo wetu ni umoja na ushirikiano badala ya mgawanyiko, majadiliano badala ya amri/mabavu, na haki badala ya visasi. Taifa la Tanzania limejengwa kwenye misingi ya amani na utulivu wa kisiasa; nguvu yoyote inayokusudia kuchafua misingi hiyo hatutokubaliani nayo.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande mwingine, tutaendelea kuviimarisha vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama ili tuhakikishe ulinzi wa mipaka yetu, na ulinzi wa raia na mali zao. Vilevile, Taifa la Tanzania litaendelea pia kutimiza wajibu wake wa kuchangia misheni za ulinzi wa amani za kikanda na kimataifa.

***Mheshimiwa Spika;***

Tumezungumzia masuala mengi, ila msingi wa mafanikio yote haya ni utawala wa sheria, uadilifu na uwajibikaji katika kila ngazi, kuanzia juu mpaka chini. Kwa msingi huo, na ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili, tutaelekeza jitihada zetu kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, ubadhirifu, uzembe, ukosefu wa nidhamu na ukosefu maadili. Ni lazima tudhibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi.

Aidha, ili kuimarisha uwajibikaji Serikalini, tutaendelea kutekeleza programu za maboresho ya utumishi wa umma, ikiwemo matumizi ya mifumo ya upimaji wa utendaji kazi. Wajibu huenda na haki, au haki huambatana na wajibu. Hivyo basi, pamoja na kuwataka watumishi wa umma kuwajibika ipasavyo, tutaendelea kuboresha maslahi yao kadri uchumi utakavyoruhusu.

***Mheshimiwa Spika;***

Vile vile, tutaimarisha uwajibikaji na utendaji wa mashirika ya umma. Kuelekea 2030, tutafanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuboresha ufanisi, uwazi na tija. Tunataka kuongeza sio tu gawio ambalo Serikali inapokea, lakini pia kufikia lengo la Mashirika na Taasisi za Umma kuchangia angalau **asilimia 10** ya mapato yote yasiyo ya kodi.

Nia yetu ni kuyajengea uwezo Mashirika ya Umma yaweze kushindana na kuwekeza nje ya Tanzania, kama mashirika mengine ya nje tunavyoyaona hapa nchini kwetu.

***Mheshimiwa Spika;***

Msingi mwingine wa mafanikio yote haya ni utawala wa sheria. Ahadi yetu ni kuwa Serikali itashirikiana kwa dhati na Mahakama ya Tanzania kuhakikisha haki inapatikana

kwa watu wote na kwa wakati. Tutaendelea kuwezesha Mahakama kwa majengo, vitendea kazi, watumishi pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA. Tunachukua hatua zote hizi ili Mhimili huu uweze kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi.

Tutasimamia utekelezaji kamili wa mapendekezo ya Tume ya Rais ya kuangalia namna ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai. Tutaendelea kufanya mageuzi na maboresho katika taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya Haki Jinai ili ziweze kukabiliana na vitendo vyote vya uhalifu.

Kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ya Sheria, ikiwemo Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) pamoja na asasi zingine ili kuwezesha upatikanaji wa huduma na msaada wa kisheria kwa wananchi, kwani katika kipindi kilichopita tumeona manufaa yake katika utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Aidha, tutakamilisha tafsiri ya sheria zetu zote kwa lugha ya Kiswahili, ikiwa ni hatua muhimu kuhakikisha wananchi wetu wanaelewa kwa urahisi sheria za nchi.

## HITIMISHO NA KUFUNGUA BUNGE LA 13

***Mheshimiwa Spika;***

Sikuweza kuyasema yote yatakayofanyika ndani ya miaka mitano ijayo kwa kuwa muda hauruhusu. Bila shaka, nitapata wasaa mwingine wa kulihutubia Bunge hili tukufu siku zijazo. Katika shughuli za kawaida za bunge, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu mawaziri nitakaowateua hivi karibuni, chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, watapata wasaa wa kufafanua kwa kina maeneo niliyoyagusia pamoja na maono ya Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Aidha, ikikupendeza, Mheshimiwa Spika, hotuba hii ikajadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, Serikali itakuwa tayari kupokea maoni, ushauri na mapendekezo yenu kwa moyo mkujunfu ili tuweze kuyafanyia kazi.

***Mheshimiwa Spika;***

Naliahidi Bunge lako Tukufu ushirikiano wangu binafsi na wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuyatekeleza yote haya kwa manufaa ya Watanzania ambao Wabunge hawa wanawawakilisha. Rai yangu kwenu ni kutoa ushirikiano wa dhati kwa Serikali. Kwa

pamoja, tutajenga Nchi ambayo mifumo inafanya kazi na miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi ili Watanzania nao waweze kufanya kazi zao kwa bidii na weledi kwa maendeleo ya Taifa letu. Namuomba Mwenyezi Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu vitakavyoachwa, bali pia kwa tabasamu la utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania.

***Mheshimiwa Spika;***

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima ya kutamka kwamba **Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa limefunguliwa rasmi**.

**Mungu Ibariki Afrika!**

**Mungu Ibariki Tanzania!**

**Mungu libariki Bunge letu na Wabunge wake!**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

# SALAMU ZA PONGEZI

Wakili Mkuu wa Serikali, **Dkt. Ally Possi** kwa Niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, anatoa pongezi **Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuchaguliwa na kuapishwa kuwa **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**



## Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi

**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**



Wakili Mkuu wa Serikali, **Dkt. Ally Possi** kwa Niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, anatoa pongezi **Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi** kwa kuchaguliwa na kuapishwa kuwa **Rais wa Zanzibar** na **Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.**

## Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi

**Rais wa Zanzibar** na **Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.**




Wakili Mkuu wa Serikali, **Dkt. Ally Possi** kwa Niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, anatoa pongezi **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba

**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

# Wajibu wa Mawakili wa Serikali Katika Kuiwakilisha Serikali Katika Mashauri Yanayofunguliwa na/au Dhidi ya Serikali



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari aliwaeleza Mawakili wa Serikali wajibu wao katika kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri yote yanayofunguliwa na/au dhidi ya Serikali ni wajibu mkubwa. "Wajibu huu ni mpana zaidi ya kwenda mahakamani, unajumuisha hatua mbalimbali ambazo zote kwa pamoja zitawezesha kutekelezwa kwa jukumu hilo kwa ufanisi, umahiri na ubora wa hali ya juu", alisisitiza Mhe. Johari. Mhe. Johari aliyasema hayo katika kikao chake na Mawakili wa Serikali kilichofanyika Arusha mwezi Oktoba, 2025 ambacho kiliandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuwakumbusha Mawakili wa Serikali wajibu wao, kujenga uelewa na kubadilishana uzoefu. Yafuatayo ni baadhi ya masuala mbalimbali ambayo yanajumuishwa kwenye wajibu huo wa Mawakili wa Serikali wa kuiwakilisha vema Serikali.

1. ***Kufanya utafiti wa kina kwenye shauri.*** *Wakili wa Serikali anatakiwa kuhakikisha kuwa kabla ya kuendesha shauri anafanya utafiti wa kina wa shauri husika kwa kuangalia Sheria, Kanuni, Maamuzi ya Mahakama na maandiko ya kisheria kuhusu shauri tajwa;*

2. ***Kuwa na Mpango Mkakati wa kuendesha shauri.*** *Wakili wa Serikali anatakiwa kupanga kuanzia mwanzo, mpango madhubuti wa kuendesha shauri. Anatakiwa kujua kwa undani hatua, muda, rasilimali na majukumu ambayo kila Wakili anayo kwenye shauri husika;*

3. ***Kufanya maandalizi ya awali.*** *Wakili wa Serikali kabla ya kuingia mahakamani, ni muhimu kufanya maandalizi ya kina ikiwa ni pamoja na kuandaa mashahidi, vielelezo, hoja za kisheria na mikakati ya maswali. Ukosefu wa maandalizi huathiri ufanisi katika kuendesha shauri;*

4. ***Kuandaa nyaraka kwa weledi na kupata idhini kabla nyaraka haijawasilishwa mahakamani.*** *Nyaraka zote za kisheria zinapaswa kuandaliwa kwa usahihi, kutumia lugha rasmi na viwango vya kitaalamu ili kuepusha mapungufu ya kisheria na kiufundi. Hii inahusisha pia kuhakiki nyaraka kabla ya kuziwasilisha pamoja na kupata idhini ya viongozi husika kabla ya nyaraka hiyo haijawasilishwa mahakamani;*

5. ***Kuzingatia mabadiliko ya sheria.*** *Sheria hubadilika mara kwa mara. Wakili wa Serikali anatakiwa kuhakikisha anazingatia mabadiliko ya kisheria na kanuni mpya zinazoweza kuathiri mashauri ya Serikali au mashauri mengine ya umma;*

6. ***Kuwa na mtazamo unaomzingatia mteja.*** *Mteja wa Mawakili wa Serikali ni Serikali. Hivyo, wakati wa utekelezaji wa majukumu Mawakili wa Serikali hawana budi kufahamu matakwa ya Serikali kwa kujua Serikali inataka nini. Kwa kutambua hilo, itawawezesha Mawakili wa Serikali kubaini namna ya kufikia adhma yake na kufahamu wanapaswa kufanya nini;*

7. ***Utekelezaji kwa wakati na ufuatiliaji.*** *Mawakili wa Serikali wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia muda wanaopangiwa na kufuatilia iwapo shauri lao linaenda sawa;*

8. ***Uadilifu na maadili ya uwakili.*** *Katika kusimamia mashauri, Wakili wa Serikali lazima azingatie viwango vya juu vya uadilifu, kuepuka mgongano wa maslahi na kuhakikisha analinda maslahi ya umma;*

9. ***Umuhimu wa ushirikiano.*** *Wakili wa Serikali anatakiwa kushirikiana na wanasheria wenzake, maafisa wa Serikali na mashahidi ili kuhakikisha shauri linaendeshwa kwa uratibu na mshikamano;*


10. ***Uwekaji wa kumbukumbu na uwazi.*** *Mawakili wa Serikali wanatakiwa kuhakikisha wanarekodi yaliyojadiliwa kwa ufanisi kwenye majalada na mifumo ya kuhifadhi taarifa za mashauri. Pia, wanatakiwa kutoa taarifa kwa viongozi wao kuhusu yaliyojiri mahakamani;*

11. ***Umuhimu wa umakini na usiri.*** *Uwepo wa baadhi ya mashauri ya Serikali hususan yenye maslahi mapana na yanayogusa hisia za wananchi wengi, Wakili wa Serikali anatakiwa kushughulikia taarifa kwa umakini na usiri wa hali ya juu ili kulinda heshima ya Serikali na kuimarisha imani ya umma; na*


12. ***Tathmini ya Matokeo.*** *Tunahitaji kufanya tathmini madhubuti pindi amri au maamuzi mbalimbali yanapotolewa na Mahakama. Kama shauri tumeshindwa tuwahi kuwasilisha Notisi ya kukata rufaa na kuandika ushauri wa kisheria wa hatua stahiki za kufuata.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Hamza Johari akimkabidhi Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. George Masaju juzuu ya sheria mbali mbali za nchi.*



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakifanya utafiti kabla ya Kwenda Mahakamani kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali.*




*“Ni kwa kuzingatia wajibu huo na mengine mengi napenda kusisitiza umuhimu wa kuiwakilisha vyema Serikali kwenye mashauri. Mashauri yanabeba taswira ya nchi yetu, yanaakisi mifumo mbalimbali ikiwemo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Hivyo tukitambua unyeti wa mashauri hayo, hatuna budi kuhakikisha kuwa tunapata uelewa madhubuti utakaotusaidia katika kuyaendesha mashauri hayo,” alisisitiza Mhe. Johari.*

**OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL**
**10 Kivukoni Road**
**P. O. BOX 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Phone: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Tovuti: www.osg.go.tz**
**Email: info@osg.go.tz**

## POSTAL ADDRESS AND LOCATION OF REGIONAL OFFICES

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 1902, 41218 DODOMA
Ministry of Constitutional and Legal Affairs - Building (UDOM)
Email: dodoma@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 130
31101 MUSOMA
Regional Commissioner's Office Building
Email: mara@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 1280
63114 MTWARA
Maadili House
Email: mtwara@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 394
33101 MWANZA
Regional Commissioner's Office Building
Email: mwanza@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 595
51108 IRINGA
Siasa ni Kilimo, Gangilonga Street
Email: iringa@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 106
35102 BUKOBA
Treasury Building (Asset Management Recovery)
Email: kagera@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 564
57101 SONGEA
Regional Commissioner's Office Building
Email: ruvuma@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 43, 37101 SHINYANGA
Regional Administrative Secretary Building,
Old District Commissioner's Office
Email: shinyanga@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 60
21101 TANGA
Mkonge House
Email: tanga@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 119
45112 TABORA
Regional Commissioner's Office Building
Email: tabora@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 202
25101 MOSHI
TRA Building - Moshi
Email: kilimanjaro@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 690
55103 SUMBAWANGA, Ukaguzi Street
Ukaguzi House, Second Floor
Email: rukwa@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 66
23101 ARUSHA
AICC Building - Arusha
Email: arusha@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 710
53107 MBEYA
Madini House
Email: mbeya@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 172
47101 KIGOMA, NHC Building, 2nd Floor,
Lumumba Street.
Email: kigoma@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
NSSF Building, Fourth Floor
MOROGORO, OLD DSM ROAD
Email: morogoro@osg.go.tz

OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
P. O. BOX 422 MANYARA,
Regional Administrative Secretary Building,
Email: manyara@osg.go.tz

***Excellence in Government Litigation***